ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tatu - Tarehe 24 Oktoba, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 41

Vitendea Kazi kwa Jeshi la Polisi Upande wa Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Kwa kuwa Jeshi la Polisi ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Muungano wa Tanzania na kwa kuwa nichombo muhimu sana kwa ajili ya ulinzi wa raia na mali zao nchi nzima na katika kila pembe ya nchi hii. Na kwa kuwa vitendea kazi muhimu vya Jeshi la Polisi kama vile helikopta vyote hivi vipo upane mmoja wa Muungano.

a) Je, Serikali inaweza kulieleza Baraza hili ni Helikopta ngapi zinamilikiwa na Jeshi letu la Polisi.

b) Je, ni helikopta ngapi zipo Tanzania Bara na ngapi zipo Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linamiliki helikopta mbili, moja kubwa na nyengine ndogo, zote hizo zipo mbili zipo cha Kikosi cha Anga kinachosimamiwa na Makao ya Polisi ya Dar es Salaam. Kwa maana hiyo helikopta hizo zipo Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, helikopta hizo licha ya kuwepo kwake Tanzania Bara lakini ni vyema ikaeleweka zinafanya kazi katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulingana na mahitaji ya wakati husika kama vile katika doria mbali mbali au wakati wa maafa au wakati wa maadhimisho mbali mbali ya kitaifa na kadhalika.

Hata hivyo, uwekaji wa vifaa hivyo unategemea mkakati wa kiulinzi lakini hauzuii kutumika wakati vinavyopohitajika katika eneo jengine katika Jamhuri ya Muungano. Lakini ninapenda pia ieleweke kuwa upo umuhimu wa helikopta kuwepo hapa Zanzibar kutokana na mazingira yetu kama kisiwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais mdogo wangu, naomba niulize swali dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa Tanzania imefanywa na nchi mbili; kwa maana ya Tanganyika au Tanzania Bara wengine wanasema hivyo na kwa upande wa pili ni Zanzibar. Na kwa kuwa mwenyewe Mhe. Waziri amekiri kwamba helikopta zilizopo ni mbili na kwa kuwa nchi mbili, ni sababu gani za msingi zilizofanya kwamba helikopta moja isikae Zanzibar na helikopta nyengine isikae kule Tanganyika. hilo la kwanza.

b) Kuendelea kuagizisha helikopta yanapotokea matatizo kama vile ajali za meli ambazo mara nyingi huwa tunazipata, kuendelea kuagizisha Tanganyika ili ije ifanye kazi Zanzibar, hali ya kuwa Tanganyika ni mdau wa helikopta zile mbili. Je, huko ni kuidhalilisha Zanzibar ndani ya Muungano huu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza ya (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba zimekaa Dar es Salaam Makao Makuu ni suala moja kuhusu masuala ya kiulinzi, mkakati wa kiulindi ndio maana wakaweka pale. Lakini kama nilivyosema kwamba upo umuhimu Zanzibar kama visiwa pia kuwa na helikopta ikiwa *station* hapa, lakini hiyo inategemea sana na uwezo wa kifedha. Kwa hivyo, ninakubaliana naye sana Mhe. Mwakilishi umuhimu wa kuwa na helikopta Zanzibar.

Tutaendelea kuwasiliana na Jeshi la Polisi katika Jamhuri ya Muungano ili kuhakikisha kadri ya uwezo utakavyopatikana iwepo na helikopta nyengine hapa Zanzibar. Kutokuwepo kwa helikopta hakusababishwi kwamba kunadhalilisha ni hali halisi ya uchumi wetu ambao uliosababisha kwa sasa kuwa na helikopta mbili na helikopta zenyewe kama nilivyosema moja ni kubwa na moja ni ndogo na hiyo ndogo haikuwa katika hali nzuri na zilinunuliwa wakati tofauti. Kwa hivyo, hata ukiileta ndogo ikawa *station* hapa kwa hali yake basi hapo ndio itaonekana kama imedhalilishwa kutokana na hali halisi ya ile helikopta yenyewe. Kwa mimi ninafikiri bado tuendelee

kuzungumza na wenzetu tuone umuhimu wa kuwepo na helikopta hapa Zanzibar ili ziweze kufanya kazi zinazohitajika.

Nam. 60

Mpango wa SUZA Kuanzisha Kitivo cha Kilimo Pemba

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Katika kipindi cha miaka ya nyuma Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilikuwa na mpango wa kuanzisha Kitengo cha Kilimo Tawi la Pemba *(Faculty of Agriculture Pemba Brach)* jambo ambalo lingesaidia sana katika kuendeleza ile dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Kilimo.

Je, mpango ule bado upo au haupo tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa Chuo Kikuu cha Taifa kina azma ya kupanua shughuli zake huko Pemba ikiwa ni pamoja na kuanzisha mafunzo ya walimu ili kupeleka huduma zake karibu sana na wananchi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kina nia ya muda mrefu ya kuanzisha mafunzo ya kilimo huko Pemba. Hata hivyo kwa 2015/2016 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Wakati Mhe. Naibu Waziri kwa umakini mkubwa anaendelea kunijibu swali langu, ninapata wasi wasi sisikii kutokana na maneno ya hapa na pale katika huu ukumbi. Kwa hivyo naomba udhibiti kidogo ili hili jibu nipate kulisikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Sawa. Waheshimiwa Wajumbe, Mheshimiwa akijibu tumsikilize, mtu anayetaka kuzungumza atoke nje akazungumze, akishamaliza arudi ndani, humu tumejia kazi maalum. *(Makofi).*

Kwa hivyo mwenye mazungumzo aende nje, baadae akimaliza atarudi ndani. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba nirejee jibu langu ili Mhe. Mwakilishi afahamu nilichokuwa nikizungumza.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kina nia ya muda mrefu wa kuanzisha mafunzo ya kilimo huko Pemba. Hata hivyo kwa mwaka 2015/2016 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kitaanza kutoa mafunzo ya ualimu huko Pemba katika Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa Mchangamdogo. Kuwepo Chuo Kikuu hapo Mchangamdogo itakuwa ni kichocheo cha kutanua shughuli zake katika nyanja nyengine kwa kadri ya uwezo na mahitaji ya nchi yatakavyoongezeka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri sana na lugha nzuri aliyotumia Mhe. Naibu Waziri katika kunijibu hili swali langu, naomba niulize swali dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Prof. Idrissa Rai pamoja na Wahadhiri wenzake pale SUZA kwa kuwa makini katika kutoa na kusimamia taaluma katika nchi yetu. Baada ya utangulizi huo naomba niulize swali dogo kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Serikali tayari imeanza mpango kupeleka *Faculty of Education Pemba Branch* pale Benjamin William Mkapa, lakini vile vile kushindwa kumuwezesha Prof. Rai na Chuo hichi Kikuu cha SUZA kuanzisha hii *Faculty of Agriculture* kule *Pemba Branch*, ninadhani itakuwa ni tatizo kubwa kwa Serikali kuweza kufanikisha ile azma yake ya kuweza kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi hii.

Je, ni lini Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Daktari Ali Mohamed Shein itaiwezesha SUZA kuanzisha *Faculty of Agricuture Pemba Branch* kusudi iweze kusibu ile dhamira yake ya mapinduzi ya kilimo katika nchi hii kwa kuweza kutoa wataalamu wa taaluma hii ya kilimo ikiwemo mambo ya *crop production* na kadhalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Ninadhani Mhe. Mwakilishi analijua hili suala la kuanzishwa tawi la Chuo Kikuu la kilimo kule Pemba na ndio maana akauliza. Mhe. Naibu Spika, SUZA waliomba sehemu ya Chamanangwe kutaka kujenga Chuo cha Kilimo kama ni tawi la Chuo Kuu cha SUZA. Kwa bahati mbaya sehemu ile ambayo waliyoomba sehemu moja ni shamba la Serikali lakini sehemu moja ni

mashamba ya wananchi ambayo pana wananchi wengi pale wanaolima. Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, kiwanja kile hakukupatikana.

Ndio maana nikasema kuwa SUZA wameanzisha haya mafunzo ya ualimu Pemba kwenye Chuo cha Mchangamdogo. Mchangamdogo na pale Chamanangwe walipokuwa wakitaka kujenga pia si mbali. Kuanzishwa kwa chuo hichi cha Mchangamdogo kutarahisisha SUZA kuweza kufikia lile lengo ambalo walitaka walifikie. Lakini kwa hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tayari tumo kwenye utaratibu wa kuandaa Rasimu ya Sheria, ikikamilika Rasimu hiyo tutaileta kwenye Baraza la Wawakilishi kuunganisha Chuo cha Afya cha Mbweni, Chuo cha Maendeleo, Utalii Maruhubi na Uongozi wa Fedha Chwaka. Kwa hivyo ile nia nzuri ya Prof. Rai Serikali inaiona na inafanya jitihada ya kuhakikisha nia ile nzuri inafikiwa.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana.

Nam. 9

Mazao ya Baharini na Mifugo kutoka Nje ya Nchi

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ikiruhusu mazao ya baharini na mifugo kama vile kuku, maziwa na samaki kutoka nje ya nchi na kuanza kuathiri wafugaji wa ndani na wavuvi.

a) Serikali imechukua hatua gani za kuwalinda wazalishaji wake wa ndani na uingizwaji wa bidhaa hizo.

b) Kwa kuwa samaki na kuku wamekuwa wakiingizwa kwa kiwango kikubwa Zanzibar, viwango vyake vya ubora imezingatiwa vipi ili kuhakikisha usalama wa afya za wananchi wa Zanzibar.

c) Sababu gani za msingi zimepelekea samaki wa maji chumvi kuingizwa Zanzibar wakati Zanzibar yenyewe imezungukwa na bahari kuanzia Mtambwe mpaka Makunduchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutufika katika hali ya uzima na afya njema. Lakini kabla ya kujibu swali kwanza nikubaliane sana na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa Serikali imekuwa ikiruhusu mazao ya baharini na mifugo kuingizwa hapa Zanzibar.

Sasa kwa idhini yako Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali Nam. 9 la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua kuwalinda wazalishaji wake wa ndani na waingizaji wa bidhaa hizo kwa kufanya tathmini ya mahitaji ya bidhaa hizo nchini na kubaini kama kuna upungufu au laa. Hapo ndipo uamuzi wa kuruhusu bidhaa hizo na kiwango cha kuingizwa kwa wakati huo unaporuhusiwa bila ya kuathiri wazalishaji wa ndani, yaani uzalishaji wa ndani unapoongezeka, uzalishaji wa bidhaa kutoka nje utapungua na uzalishaji wa ndani ukipungua basi na bidhaa kutoka nje zitaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Chakula na Madawa na Vipodozi iliyo chini ya Wizara ya Afya ndio wenye mamlaka ya kuhakikisha chakula chote kinachoingizwa nchini kinakidhi vigezo vya viwango vilivyowekwa na Bodi hiyo.

Aidha, kabla ya bidhaa hizo kuruhusiwa kuingizwa nchini kwa matumizi ya chakula, wahusika hutuma maombi kwetu na kuonesha kiwango cha bidhaa kinachotoka kuingizwa nchini, hapo ndipo huwasiliana na Bodi hii ya Chakula ili kufanya uchunguzi wa bidhaa hizo na kama imekidhi masharti yaliyotakiwa na kuwa ni matumizi salama kwa binadamu basi huwa tayari kuruhusu kuingia nchini.

Mhe. Naibu Spika, sababu za msingi zinazopelekea kuingizwa kwa samaki wa maji ya chumvi hapa Zanzibar, wakati Zanzibar yenyewe imezungukwa na bahari ni kutokana na upungufu uliopo wa samaki unaopatikana hapa nchini kulingana na mahitaji ya wananchi na wageni katika hoteli za kitalii. Wastani wa pato la samaki wanaovuliwa nchini ni kilo milioni ishirini na saba laki tisa tisini na nne elfu, mia tano na tisini na sita kwa mwaka. Kwa kiwango hicho ni wastani wa kilo ishirini kwa samaki kwa kila mtu kwa mwaka mmoja.

Mhe. Naibu Spika, hivyo ili kukidhi mahitaji ya viburudisho vya kujikinga mwili *(protein)* kwa wananchi kwa kuzingatia kuwa samaki ndio chanzo cha *protein* halisi kwa wananchi wetu au urahisi ukilinganisha na bei ya vyanzo vyengine kama nyama, ndio maana samaki huingizwa nchini ili kukidhi mahitaji yao. Ni vyema tukumbuke kuwa kuna baadhi ya wakati mahitaji ya samaki huongezeka nchini kama vile mwezi Mtukufu wa Ramadhani na wakati wa msimu mkali wa upepo wa Kusi na Kaskazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ule mpango wake wa MKUZA, ina mpango wa kupunguza umaskini na wananchi kujiongezea kipato, *I mean product reduction income generative*. Mhe. Naibu Spika, kwa mnasaba huo zaidi ya Wazanzibari asilimia 60 wamewekeza maisha yao katika masuala ya kufuga kuku hawa na ng'ombe na uvuvi baharini.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba umesema kuwa kwa mujibu wa takwimu ulizotoa kama samaki wanaongezeka lakini kuku hukutaja na mifugo mengine. Je. Mhe. Naibu Spika, kuendelea kuagiza kuku hawa PADUU kutoka Brazil huku wafugaji wa Muyuni, Vitongoji, Makunduchi wakiendelea kuzalisha kuku kwa wingi, huko itakuwa kuwapunguzia au kuwaongezea umaskini Wazanzibari wa nchi hii. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mhe. Saleh Nassor Juma kwa maswali yake muhimu sana ya kutetea wananchi wetu. Lakini kwa taarifa nilizokuwa nazo mwaka 2013 wafugaji wetu wa ndani walizalisha kuku tani elfu saba na nne point nane, sawa na kilo laki saba na nane, mia nane na thalathini na tisa kwa mahitaji ya tani elfu nane, mia tisa na nane sawa na kilo 8,908,000 wakati idadi hiyo ni ndogo sana ambayo inahitaji kwa kulingana na soko letu.

Lakini soko likoje Zanzibar la kuku wetu, sasa soko ni dogo sana kulingana na mahitaji yetu halisi. Kwa hivyo, tunaona ni bora kuona kile kigezo au kipengele ambacho tumekiwacha pale ili tuweze kujaliza. Lakini serikali kupitia mpango wake huu wa mkuza, sasa inakuja na wizara imeomba pesa serikalini ili kuwawezesha wananchi waweza kuziba lile pengo, ili baadaye serikali inaweza kupiga marufuku kuagiza pale kuku wale wanaotoka nje.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kutupa afya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakumbuka kwamba bajeti ya mwaka juzi, nililizungumzia sana suala hili la makuku mabovu, nilisema hivyo hivyo makuku mabovu. *(Makofi)*

Sasa hivi tunaletewa masamaki mengine mabovu tunakubali. Natoa tahadhari Mhe. Naibu Spika, bajeti inayokuja sipitishi. Namuomba Mhe. Naibu Waziri anipe majibu ya uhakika, walichukua hatua gani ambayo walisema kwamba kuku wale wakimalizika hawatoagiziwa tena, lakini kila kukicha yanamiminika makuku mabovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Mama Asha Bakari Makame kwa swali lake zuri lenye kutia afya zaidi.

Lakini nataka kusema bado serikali imeona kuna biashara huria, lakini mbali ya kuwa na biashara huria, wale kuku wanaoingizwa tumesema mahitaji yetu ni makubwa mno, kulingana na uzalishaji wetu wa ndani, ndio serikali ikaamua tuweze kuziba lile pengo ili baadaye basi baada ya wizara kuwawezesha wafugaji wake wa ndani na kuziba lile pengo, basi hatutaagiza tena, au tutatafuta njia ya kuweza kuwazuwia ili wasiletwe hapa. Lakini sasa hatuwezi kuwazuwia kwa sababu biashara ni huria na hiyo ndio sera ya serikali.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu, alitueleza kwamba uzalishaji wa ndani ukiongezeka, ndio utapunguza suala zima la uagiziaji na kinyume chake.

Sasa sisi Zanzibar moja kati ya mipango yetu ni kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji. Mhe. Naibu Waziri kati ya haya mambo ambayo nitakutajia, hebu nieleze ni lipi ambalo ndio tatizo letu. Je, tuna tatizo la udhaifu wa sera, tuna tatizo la kisheria, tuna tatizo la uvivu wa watu wetu, tuna tatizo la kibajeti au tatizo ni usimamizi wa serikali. Ni mambo gani kati ya hayo ambayo ndio yanayotuathiri Zanzibar na utakaponitajia moja Mheshimiwa naomba unipe jawabu, kwamba je wizara yako imejiandaa vipi kukabiliana na tatizo hilo. Nashukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza tu niseme tatizo lililokuwepo ni tatizo la kisera. Sera kwa sababu gani, kwa sababu moja ya sera yetu kuwa na biashara huria katika Zanzibar na hatutaweza kumzuwia mtu yeyote kuleta bidhaa hapa ni lazima alete. Lakini serikali imefanya nini. Nilisema katika jibu langu la msingi sana. Serikali sasa hivi imekuja na sera hii ya kutaka kuwawezesha wafugaji ili kuziba lile pengo, baada ya kuziba lile pengo, tutatafuta njia sasa ya kuzuwia vile vitoweo ambavyo vinatoka nje ili tuweke sawa na wafugaji wetu wawe na afya zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri, Katibu tuendelee. Mhe. Saleh Nassor Juma. Wajumbe utulivu tufahamiane.

Nam. 51

Ubovu wa Barabara ya Daraja Bovu Juu (Uholanzi)

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Eneo la Daraja Bovu juu (Uholanzi)lililopo katika Manispaa ya mji wa Unguja lina wakaazi wasiopungua 4000, ambao hutegemea soko la Mjini kwa ajili ya shughuli zao za kila siku, na kwa kuwa barabara inayounganisha wakaazi hao na barabara kuu ni mbovu mno, kiasi ambacho haipitiki na inaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi husika, hususan wajawazito wanaotoka Darajabovu juu hadi njia kuu ya Mtoni/Amani.

Je, ni lini serikali itawakomboa wananchi hawa kwa kuwajengea barabara hiyo ambayo haizidi kilomita tatu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, swali nililonalo mimi ni swali nambari 55, Mheshimiwa Mjumbe kasema 56, 56 sina wala sijaulizwa. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Spika: kuna 55.

Nam. 55

Ukosefu wa Usafiri wa Uhakika kwa Wanasheria wa DPP Pemba

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Uhaba wa usafiri katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kanda ya Pemba, kwa kiasi fulani umekuwa ukisababisha kesi zichelewe katika Mahakama mbali mbali za Pemba, kwani gari moja lililopo haliwezi kuhudumia wanasheria katika Mahakama zote za Pemba kwa siku moja.

Je, ni lini serikali itawapatia wanasheria hawa wa DPP Afisi ya Pemba usafiri wa ziada, ili kesi katika Mahakama za Pemba zisikwame, ukitilia maanani kwamba "haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa".

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mjumbe swali lake nambari 55 kama ifuatavyo:

Katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba ziko gari mbili kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa mashtaka. Moja ndilo linalotumika kwa shughuli za kuwapeleka wanasheria katika Mahakama za Wilaya ya Mkoa wa Kaskazini kwa siku tatu kila wiki, kuanzia Jumanne hadi Alhamis.

Kwa upande mwengine wa Mahakama za Wilaya ya Mkoa wa Kusini hutumika gari nyengine kwa siku tatu vile vile, kuanzia Jumanne mpaka Alhamis. Gari hizi kwa ujumla haziko katika hali ya kuridhisha, ambapo pia hutumika kwa shughuli hizo za Mahakamani, pamoja na kutumiwa na Mwanasheria dhamana wa uendeshaji mashtaka wa Pemba.

Endapo gari hizo zinapokuwa Mahakamani Mwanasheria dhamana hulazimika kusubiri gari hizo zirudi kutoka Mahakamani ndipo na yeye aweze kutumia gari hizo kwa shughuli nyengine za kiofisi.

Ni kweli kwamba gari hizi mbili ni za zamani sana, tokea kuanzishwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, na pia hazitoshelezi katika kufanya shughuli za mashtaka katika Mikoa hiyo.

Hata hivyo, tokea kuanzishwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, hapajawahi kutokea hata siku moja, kuwa wanasheria wakakosa usafiri huo kwa ajili ya kwenda Mahakamani. Kwa hivyo, sio sahihi kwamba kesi huchelewa kutokana na uhaba wa usafiri, ila kuna sababu nyengine ambazo hazitokani na kukosa usafiri. Sababu zenyewe ni kama vile kutokuhudhuria kwa mashahidi, kutokukamilika kwa ushahidi na uchunguzi, wazee au jamaa wa wahusika kukataa kutoa ushahidi Mahakamani na kadhalika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri katika masuala haya ya katiba, na mimi naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa swali hili nimeliuliza baada ya kufanya utafiti wa kina na upembuzi yakinifu na kuona kwamba gari liliopo ni moja tena chakavu. Siku linakwenda na siku nyengine linashindwa kwenda na kwa sababu yeye mwenyewe kakiri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa kwa mujibu wa hao hao wanasheria kwamba haki ikichelewa kutolewa ni sawa sawa na kwamba haikutolewa kabisa. Kwa kuwa kuna ushahidi wa kutosha unaoonesha kwamba gari hili siku nyengine likienda Mkoani, siku nyengine linashindwa kufika Wete na wanasheria na kesi zinakwama kwama.

(a) Je, haoni kwa kuendelea kubaki na gari moja ni kuifanya nchi yetu hii Zanzibar ikaenda kinyume kidogo, kwa sababu wanachelewesha kesi, ikaenda kinyume kidogo na utawala wa sheria.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar imetia mkataba mambo ya haki za binadamu, kwa hivyo kuendelea kurundika makesi pale katika Mahakama zetu, kutokana na uzembe huu wa kuwa gari ni bovu au chakavu, haoni kwamba tunakiuka misingi ya haki za binadamu, na

(c) Kwa kuwa wafanyabiashara wa kawaida tu wanamiliki gari katika shughuli zao. Je, kuendelea kukosa gari kwa serikali yetu katika ofisi nyeti kama hii, haoni kama ni kuidhalilisha nchi yetu. Ni lini serikali italeta bajeti ya magari pale katika Afisi ya DPP pale Pemba, ili tuipitishe kwa shwange, ili magari yanunuliwe pale na hatimaye kesi ziende vizuri pale.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema ni kwamba Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba kuna gari mbili sio moja. Nalisema hili kwa uhakika, kwa sababu kiasi mwezi mmoja nyuma mimi nilikuwepo huko.

Mhe. Naibu Spika, nakubali kwamba gari sio nzuri sana, lakini pia nathibitisha kusema kwamba hata siku moja mwanasheria au mwendesha mashtaka hajakwama kwenda Mahakamani kwa sababu ya ubovu wa gari, hata kama gari ni mbovu basi tunahakikisha kwamba gari nyengine inapatikana au inakodiwa, ili mwendesha mashtaka afike Mahakamani.

Lakini kama nilivyosema kwamba kucheleweshe kesi haitokani na mwendesha mashtaka peke yake. Kuchelewa kwa kesi ina mambo mengi Mhe. Naibu Spika, kwanza kama nilivyosema, inaweza ikawa uchunguzi

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mazungumzo yamekuwa mengi, tumsikilize Waziri anajibu maswali.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Inaweza ikawa uchunguzi, inaweza ikawa wahusika wenyewe, inaweza ikawa mashahidi nao wana matatizo ya kutoa ushahidi. Kwa hivyo, kwa misingi hiyo kesi lazima iahirishwe. Kwa hivyo, sio waendesha mashtaka wanaosababisha kurundikana kwa kesi, lakini ni jamii wenyewe ambayo inahusika katika kusababisha kurundikana kwa kesi.

Lakini jambo la tatu ni kwamba kutokana na upungufu huu, hata katika bajeti yetu ya mwaka jana, kama anakumbukumbu, tuliomba Baraza lako tukufu liidhinishe suala la gari za waendesha mashtaka, lakini kutokana na ufinyu wa

bajeti fedha hizo zilikatwa. Ninachopenda kusema ni kwamba bado tutaendelea kutafuta misaada na kutafuta bajeti ambayo inaweza ikatusaidia kwa kutafuta gari mpya sio kwa waendesha mashtaka tu, lakini hata katika sehemu nyengine au idara nyengine za wizara yangu.

Nam. 51

Ubovu wa Barabara ya Daraja Bovu Juu (Uholanzi)

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Eneo la Daraja Bovu juu (Uholanzi)lililopo katika Manispaa ya mji wa Unguja li9na wakaazi wasiopungua 4000, ambao hutegemea soko la Mjini kwa ajili ya shughuli zao za ikila siku, na kwa kuwa barabara inayounganisha wakaazi hao na barabara kuu ni mbovu mno, kiasi ambacho haipitiki na inaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi husika, hususan wajawazito wanaotoka Darajabovu juu hadi njia kuu ya Mtoni/Amani.

Je, ni lini serikali itawakomboa wananchi hawa kwa kuwajengea barabara hiyo ambayo haizidi kilomita tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 51 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, barabara ya ndani ya Darajabovu ilioelekea Uholanzi ni miongoni mwa barabara ambazo ziko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Lakini kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri zetu, wizara yangu iko tayari kuifanyia matengenezo hayo kwa kutoa wataalamu na zana za kazi, iwapo uongozi wa jimbo hilo utachangia gharama za matengenezo ya barabara hiyo kulingana na tathmini itakayofanywa.

Michango ya matengenezo ya barabara kama hizo, imeshawahi kufanywa na viongozi wa majimbo mbali mbali. Miongoni mwao ni kiongozi wa jimbo hilo hilo la Magogoni, kiongozi wa Mwanakwerekwe na Jimbo la Mpendae kwa kutumia fedha za mfuko wa Jimbo, na barabara hizo tayari zimeshafanyiwa matengenezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba tu Mheshimiwa Mwakilishi aendelee na utaratibu wetu ule ule, wa kukutana na kushauriana, ili kuweza kuona ni namna gani tunaweza kuwaondolea usumbufu wananchi wetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya mdogo wangu hapa Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Issa Gavu, pamoja na majibu yake mazuri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa uongozi wa jimbo hauruhusiwi kukusanya kodi na inayokusanya kodi ni serikali, na kwa kuwa Zanzibar tuna mpango wa kukupunguza vifo vya mama na mtoto, *reduction of mother child mortality rate,* katika maeneo yetu yote, likiwemo lile eneo la Darajabovu kule sehemu za Uholanzi.

Kwa kuwa wazazi wengi huwa wanapata taizo kutokana na barabara ile, ambapo mara nyingi akina mama hulazimika kujifungua barabarani, huku watoto wakiwa katika hali mbaya, au wazazi wenyewe wakiwa katika matatizo makubwa ya uzazi na hivyo kuathiri afya zao.

(a) Je, kuendelea kuwasubiria viongozi wa Jimbo watengeneze, huku serikali inayokusanya kodi ikiwaachia akina mama na watoto wakiathirika katika barabara ile mbovu, si kuwadharau walipa kodi wa nchi hii.

(b) Ni lini Mhe. Waziri wizara yako itapita katika barabara ile na kufanya tathmini ya kina na upembuzi yakinifu wa *renovation* ya ile barabara, kusudi tupite humo barabarani tukiomba watu watusaidie, ikiwa serikali itakuwa imeshindwa, tuwaombe watusaidie ili itengenezwe ile barabara kusudi wazazi wapate kufika hospitali haraka kwenda kujifungua, badala ya kuathirika pale katika barabara bovu lile huku watoto wakiwa katika hali mbaya baada ya kusumbuliwa katika magari mabovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakilishi anachokiuliza ni kwamba serikali ndio inayokusanya kodi na viongozi wa jimbo hawakusanyi kodi. Kwa hivyo, kwa mawazo yake ni kwamba kwa sababu serikali ndio inayokusanya kodi na barabara hizi serikali izijenge.

(a) Serikali hatujakataa kujenga, lakini kwa mujibu wa sheria tulizojipangia sisi wenyewe, serikali hailazimiki moja kwa moja kwenda kuzijenga barabara hizo. Halmashauri ndizo zenye jukumu la msingi kisheria, kusimamia na kujenga barabara hizo. Kwa kutambua kwamba Halmashauri zetu uwezo wake wa kifedha ni mdogo, tumekubaliana nao, kwamba sisi wizara tuko tayari kutoa msaada wa vifaaa na wataalamu wetu,

na wao watusaidie gharama ili tuweze kujenga kuondosha usumbufu wanaoupata wananchi wetu.

Kwa bahati nzuri katika Jimbo hili la Magogoni, jambo hili sio geni, tayari kuna njia karibu tano, ndani ya jimbo hili hili. Ulikuja uongozi tukakaa tukazungumza nao tukakubaliana, tukenda tukashirikiana na tayari huduma ile ikawa imepatikana. Imani yangu ni kwamba utaratibu ule ule tulioutumia mwanzo, bado nafasi ya viongozi hao ipo waje tutashirikiana nao ili kuondosha usumbufu na kina mama wanaojifungua wasipate usumbufu kama ambavyo hivi sasa inajitokeza.

(b) Lini serikali itafanya tathmini. Tutafanya tathmini baada ya kukutana na wenzetu wadau hawa ili tuweze kujua, kila mmoja *commitment* yake ipi. *Commitment* ya serikali iko wazi, tuko tayari kutoa utaalamu na vifaa na wenzetu wakishakubali kwamba wako tayari kuchangia gharama, tutakwenda tutafanya tathmini ili tufanye kazi ya kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru na kumfahamisha ndugu yangu Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri kwa maelezo yake mazuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi naona tufike pahala tuwe wakweli katika Baraza la Wawakilishi. Je, mimi naona kama serikali kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hawakuwa wakweli katika kutengeneza barabara za ndani, hata wakipewa pesa wanazila na ushahidi upo, sio suala la Darajabovu tu. Suala lote upo ushahidi wa kutosha, mpaka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kachukua dhamana ya kuchukua barabara za ndani, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imechukua pesa wakala na sio wakweli katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika: Uliza swali.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Swali langu ni je, Mhe. Naibu Waziri ni kusema ukweli kwamba barabara za ndani kwa kupitia wizara yake wameshindwa kutekeleza, hata kama pesa zipo.

Mhe. Naibu Wizari wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Zanzibar tuna matatizo makubwa sana hasa kwa barabara zetu za ndani na kweli serikalini mzigo huu umetuzidi. Lakini kwa mujibu wa sheria zetu wenyewe tulizojipangia ukisoma *cap* 134 sheria ya mwaka 1958 pamoja na mabadiliko tuliyoyafanya mwaka 2013, bado jukumu la barabara hizi ndogo ndogo zinabakia kwamba ni jukumu la Halmashauri zetu.

Sisi kama wizara tunachokifanya ni mchango kama kuna pahali mchango wetu wa vifaa pamoja na wataalamu haujafika, basi ni jukumu la mwakilishi au kiongozi yeyote kuja na kuzungumza, ili tuweze kupata shufaa na ufumbuzi wa tatizo hilo. Sasa kuna maeneo ni kweli tumechukua fedha na tumekwenda kutoa huduma bado hazikukamilika, lakini maeneo hayo hayo serikali kwa kutumia nguvu zake zile zile tayari kuna huduma hizo za barabara zimepelekwa.

Kwa mfano, kama swali alilouliza swahiba wangu Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali ni kweli barabara ya Pagali haikukamilika na ina urefu takribani kilomita saba na tumefanya kilomita tano, lakini ndani ya jimbo hilo hilo barabara pacha ya Pagali ina urefu wa kilomita saba, tumejenga kilomita tano kwa kiwango cha lami.

Kwa hivyo, imani yetu kwamba wananchi watakuwa wanapima na kuona, pale serikali inapokuwa na uwezo basi tutakuwa tunafanya na pale tusipo na uwezo tutaendelea kushirikiana na viongoni. Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Mjumbe aamini kwamba sote tuna lengo moja na wala hatuna sababu ya kugombania fito tunajenga nyumba moja ya kuharakisha maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Naibu Waziri pamoja na maelezo yake ya kuwa barabara hizi zina dhana ya watu wa jimbo. Lakini naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kwa sababu kuna kuwa na kwa sababu barabara hii inayozungumzwa ya Uholanzi ni mbaya sana, yaani haipitiki.

Vile vile kuna wakaazi wengi ambao wanahitaji kusaidiwa na kwa kuwa viongozi wao wa jimbo bado hawajawa tayari. Je, haoni Serikali Kuu kupitia Mfuko wa Barabara kuwasaidia hata kuwawekea kifusi, ili wanawake wajawazito wakapata shufaa kidogo ya kupelekwa hospitali. Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo je, ni lini watawasaidia wananchi hawa, kwa ajili ya kupata shufaa kidogo wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, tunatambua kwamba Mfuko wa Barabara upo na fedha kiasi zipo. Lakini Mfuko wa Barabara huu, ningeomba kwa mambo mengine kama haya basi tuendele kuendeleza utaratibu wetu wa viongozi husika wa majimbo pamoja na viongozi wetu wa Halmashauri tuendelee kusaidiana na wizara yetu, kwa ajili ya kufanya kazi kama hizi.

Mfuko wa Barabara utatusaidia zaidi pale ambapo kuna haja ya lazima ya kuweza kutoa msaada huo. Kwa mfano, hivi majuzi mradi wetu wa Barabara ya Jendele/Cheju, Jumbi/Koani umekamwa, kwa sababu ya fedha za mfadhili hazijafika, hivyo Mfuko huu wa Barabara umeweza kuisaidia serikali kwa kuikopesha kwa ajili ya kwenda kunusuru mradi ule uendelee, ili zitakapokuja fedha za mfadhili ziweze kutumika.

Kwa hiyo, imani yetu ni kwamba fedha za Mfuko wa Barabara ziendelee kutumika kwa mujibu wa sheria yake na panapokuwa na haja ya lazima tutaendelea kuwaomba watuazime, ili serikali itakapopata fedha turejeshe. Lakini kwa mfumo wa hizi barabara za ndani, basi tunaomba tu tuendelee kushirikiana baina ya viongozi, Halmashauri pamoja na wizra yetu tuko tayari kutoa msaada wa vifaa na wataalamu wetu.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Katibu tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Jaku Hashim Ayoub): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub na kwa idhini yake naomba swali Nam. 27 kuliondoa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, kuliondoa hebu sikusikia vizuri.

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Jaku Hashim Ayoub): Mhe. Naibu Spika, kuliondoa.

Nam. 27

Ahadi ya Malipo ya Posho kwa Watendaji wa Mahakama ya Ardhi

(Mheshimiwa Mjumbe, aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Naibu Spika: Swali limeondolewa. Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Katibu.

Nam. 48

Mabwanashamba katika Ardhi za Maweni

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Wataalamu wa kilimo waliowezeshwa katika kufanya kazi zao ni miongoni mwa mambo ya msingi kuzingatiwa katika kuimarisha uchumi wa taifa lolote linalotegemea kilimo katika uchumi wake. Kwa kuwa wakulima wengi

wanaotegemea kilimo cha maweni katika ukanda wa mashariki wa kisiwa cha Pemba hutumia sana kuchoma moto misitu katika kilimo chao, jambo ambalo hupelekea uchafuzi pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Kwa kuwa hutegema sana kilimo cha zao moja katika ardhi hiyo hiyo miaka nenda miaka rudi (*mono culture*), jambo ambalo linaharibu ardhi pamoja na kuteremsha kipato chao.

Je, ni lini serikali itaajiri mabwana shamba wa kutosha katika ardhi za maweni, kwa maana ya maeneo ya Makaani, Vitongoji, Muambe na Micheweni.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba mabwanashamba na mabibishamba ni wafanyakazi ambao wana utaalamu wa kutoa huduma zao pahala popote watakapopangiwa kazi iwe maweni au katika aina nyengine ya ardhi.

Kaitka kipindi hiki cha miaka miwili cha 2012/2013 na 2013/2014 serikali imechukuwa juhudi za makusudi za kupunguza tatizo la uhaba wa mabibishamba na mabwanashamba, ambapo wafanyakazi 54 wameajiriwa.

Aidha zoezi hili litaendelea mpaka pale idadi inayohitajika itakapokamilika na kila ambapo wizara itakapopata nafasi za ajiri hizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyonge kama ifuatavyo. Kwa kuwa kilimo hichi cha maweni ndio mkombozi wa ukanda mzima wa mashariki kule Pemba kuanzia tangu Muwambe mpaka Micheweni. Vile vile kwa kuwa uharibifu wa mazingira umekithiri jambo ambalo linateremsha sana kipato cha wananchi kule katika maeneo hayo.

Je, Mhe. Waziri ana mpango gani sasa wa kutoa nafasi za masomo kwa watu wa ukanda wa mashariki kutoa *first priority* kwa kuwapatia masomo au mafunzo vijana wa kule kusoma taaluma ya kilimo, ili hatimaye wananchi wale kuweza kuwapunguzia au kuepukana na tatizo hili la maafisa kilimo ambao wangetusaidia sana kupata kuendeleza maisha yetu kule.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mjumbe kwamba tutachukua ushauri wake kwa kuwapa *priority* watu ambao walioko katika ukanda huo, ili kuongeza masomo, kwa sababu masomo wanapatiwa, isipokuwa ni kuweka *priority* makusudi ya kuwapa masomo ya kukinga mazingira ambayo hayo aliyoyataja.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii, pia nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili kwa majibu yake mazuri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Hivi ni lini serikali, kwa sababu serikali ina majukumu ya kuwasaidia wananchi wake mbali mbali, kwa kuwa serikali hiyo ndio yenye dhamana ya wananchi wake kwa mambo tofauti. Je, ni lini serikali itaweka Vituo Maalum vya Mabwanashamba au Mabibishamba, ili mkulima anapomuhitaji ampate kwa urahisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kusema kwamba lini tutaweka utaratibu huo. Lakini ushauri wake tutauchukua, ili kwenda kukaa na kuona kwamba kufanya utaratibu wa kuweka kituo kimoja ambacho tutamuweka huyu bwanashamba mmoja wale ambao wanamuhitaji wajue bwanashamba huyu yuko pahala maalum. Lakini hatuwezi kumwambia kwamba ni siku fulani, isipokuwa tutafanya utaratibu huo, tutakaa kwa kushauriana na ikiwa kuna uwezekano wa kufanya hilo basi tutafanya *Inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika: Swali la mwisho la nyongeza Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mimi nikaweza kuuliza swali langu dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kwa kila awamu wanawaajiri mabwanashamba na mabibishamba na wakulima wengi wa vilimo vya maweni wanasikitika sana kwa kutokuwapata hawa mabwanashamba na mabibishamba.

Hivi baada ya kuajiri kwenu mgao wenu ukoje katika ima munawagawa hawa kwa majimbo au shehia, sasa kama kwa kila jimbo hivi jimbo moja linaweza kupata mabwanashamba wangapi kutokana na shehia tulizonazo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, katika uajiri tunapoomba tunajaribu kutizama wapi kuna matatizo zaidi ya upungufu wa mabwanashamba au mabibishamba, kwa hiyo kule ndiko tutakapokupa nguvu hususan sehemu ya Pemba, yaani hivi sasa hili tatizo ndio kubwa.

Kwa maana hiyo, hata safari hii ambapo tumeomba na tunachotaka ni kwamba tuliomba kwa Unguja, lakini tutawagawa, ili tuwapeleke na Pemba ambapo ndio kunako tatizo hilo. Kwa mfano, tukiangalia Vitongoji ambapo ni shehia ambayo ina bwanashamba mmoja ambaye anashughulikia sehemu mbili, yaani Kibokoni na Vitongoji kutokana na ule ubaha tulionao. Kwa hivyo, huyu bwana Juma Khamis Mwalimu anashughulikia shehia mbili.

Nam. 15

Ongezeko la Idadi ya Vifo Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Jaku Hashim Ayoub):

Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo Zanzibar, zinaonesha kuwa kumekuwepo na ongezeko la vifo Zanzibar na kufikia watu 1648 kwa mwaka, kati ya watu hao wanawake ni 760.

(a) Je, ongezeko hilo linasababishwa na nini.

(b) Kwa kuwa wananchi wengi hawana utaratibu wa kupima afya zao kabla ya kuanza kuugua, serikali imechukuwa hatua gani za kuelimisha wananchi wake kupima afya zao kila mwaka kwa kuzingatia kinga ni bora kuliko tiba.

(c) Je, ni maradhi ya aina gani hadi sasa yanaongoza kwa kusababisha vifo Zanzibar na hatua gani zimechukuliwa kukabiliana nayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa hapa wazima wa afya kwa siku ya leo ya Ijumaa.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, naomba ieleweke kuwa sababu kuu zinazosababisha ongezeko kubwa la vifo sio maradhi yanayoambukiza, isipokuwa ni maradhi yasiyoambukiza nayo hutokana na mambo mbali mbali ambayo yanaisibu jamii yetu.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara kupitia kitengo chake kipya kilichoanzishwa cha *Non Communicable Disease*, yaani ni Kitengo cha

Maradhi ambayo hayaambukizi, kimekuwa kikitumia njia tofauti za kuelimisha jamii zikiwemo njia zifuatazo:-

(i) Kuelimisha wananchi kuwa wanatakiwa angalau mwaka mara mbili kupima afya zao nayo ni *basic test* kama vile kupima *pressure*, sukari, uzito na mambo mengine yanahusiana na hayo.

Pia kitengo hicho kimetumia njia ya kuonesha filamu maalum, ambayo inatoa elimu ya kutosha juu ya maradhi yasioambukiza na kutoa msisitizo na umuhimu kwa wanajamii wote kuwa na utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara kabla ya kuanza kuugua na kufuata mtindo mzuri wa maisha, ambao kwa asilimia kubwa utaweza kuwafanya wananchi waweze kujiepusha na maradhi yasioambukiza.

Miongoni mwa maradhi yasioambukiza ni *high blood pressure* ama *pressure* ya juu, *low blood pressure* (*pressure* ya chini), *organs failures* kama vile ku-*fail* kwa *kidney* na *pancreas* ambako kunasababisha pia kuleta maradhi ya kisukari, ambayo ni mengi. Vile vile maradhi hayo pia husababisha kupa *stroke* na siku hizi za hivi karibuni huonekana zaidi kwa maradhi ya kansa kushamiri kwa akinamama na akinamama.

Pia kitengo hicho kimeendelea kuonesha filamu katika shehia tofauti za Unguja na Pemba, kwani imetambulikana kwamba kupima kwa mwaka mara mbili ni bora zaidi kuliko kusubiri kuumwa, kinga ni bora kuliko tiba na kupima ni sehemu ya kinga.

(ii) Jengine ni kutumia vyombo mbali mbali vya habari kama vile redio, *television*, magazeti, mabango na vipeperushi juu ya vihatarishi vinavyopelekea watu kupata maradhi yasioambukiza hususan shinikizo la damu (*blood pressure*), maradhi ya kisukari na saratani na kuelimisha jamii zaidi juu ya maradhi haya.

Mengine ni kufanya mikutano ya uhamasishaji katika wilaya na shehia zote za Unguja na Pemba kupitia Kamati Maalum zilizoundwa za Afya kupitia Masheha, ambao Wawakilishi nao huwa wanajumuishwa katika kamati hizo zikiongozwa na watendaji wa wilaya pamoja na Masheha na Madiwani.

Lengo kuu ni kuwaelimisha washiriki wakiwa wao ni viongozi katika jamii zao waweze kueneza elimu kwa wananchi kwa kushirikuana na wataalamu wa afya, ili jamii iweze kubadilisha mtindo wao wa kimaisha na kuwa na utamaduni wa kupima afya zao angalau mwaka mara mbili kabla na pia wasisubiri maradhi mpaka yatakapojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kuwapatia semina maalum waandishi wa habari wa vyombo tofauti vya serikali na binafsi kwa Unguja na Pemba, ambapo lengo la semina hiyo ni kuwapa elimu juu ya maradhi yasioambukiza na kujua vihatarishi vinavyopelekea mtu kupata maradhi na njia sahihi za kujikinga, ili kwa nafasi yao waweze kufikia elimu hiyo moja kwa moja kwa jamii.

(c) Mhe. Naibu Spika, maradhi yanayoongoza kwa kusababisha vifo Zanzibar ni kama yafuatayo:-

- Magonjwa ya moyo ikiwemo shinikizo la damu/presha na kiharusi haya yamo katika kundi moja (hypertension and stroke) inaongoza;
- Kisukari;
- Saratani ya shingo ya kizazi na matiti kwa wanawake na saratani ya tezi dume kwa wanaume (*cervical, breast and prostate cancer*);
- Magonjwa sugu ya njia ya hewa.

Lakini naomba isisahaulike katika hii idadi ya takwimu iliyotolewa 1648, kwamba vifo 406 vinatokana na ajali za barabarani. Kwa hiyo, ni vifo 1242 tu vinavyosababishwa na maradhi, lakini 406 vinatokana na ajali za barabarani.

Mhe. naibu Spika, hatua zilizochukuliwa kukabiliana na maradhi hayo ni kama ifuatavyo:-

- Kuanzisha Kitengo Maalum kinachoratibu na kufuatilia kwa karibu sana magonjwa yasiyoambukiza (*Non Communicable Disease*), ambao wao ndio hivi sasa wanajaribu kukusanya takwimu sahihi ya maradhi haya pamoja na ongezeko lake kwa hapa Zanzibar;
- Kununua vifaa tiba na vifaa kinga, ili kusogeza huduma za kupima karibu na wananchi kupitia vituo mbali mbali vilivyokuwepo Zanzibar yaani Unguja na Pemba, jumla yake ni vituo 138 navyo ni kuvipatia BP *machine* ili mgonjwa anapokwenda kupata vipimo angalau vile vipimo vya chini kabisa anaweza kupata. BP *machine*, vifaa ya maabara, vifaa vya kupimia uzito, vifaa vya kupimia damu ya sukari pamoja na mkojo. Pia na kufanya njia nyengine za *check up* kwa vipimo mbali mbali.

Lakini pia kituo hichi cha NCD kinaimarisha mifumo ya afya pamoja na kutoa taaluma kwa jamii ili waweze kujikinga namagonjwa yasiyoambuzikiza, kwani ni magonjwa ambayo kiasi kikubwa yanaweza kuepukika iwapo watu watabadilisha mfumo wa maisha, ikiwa pamoja na kufanya mazoezi, kuacha kutumia pombe pamoja na tumbaku, na kula mto uliokamilika ambao unatokana na vyakula vya asili. Hivi sasa vyakula vingi vya asili vimeachwa kutumika Mheshimiwa pamoja na kupunguza mlo wa unaotumia mafuta kwa wingi.

Kufundisha wafanyakazi wa vituo vya afya na hatimae kuanzisha clinic maalum zinazotoa huduma za kupima afya na kutoa ushauri wa kitaalam na elimu kwa jamii kupitia njia mbali mbali.

Mwisho ni kuongeza upatikanaji wa huduma za wapimaji kutoka hospitali tatu za Unguja yaani Mnazi mmoja, Kivunge na Makunduchi hadi kufikia vituo 26 ambavyo vitatoa huduma hizo, na Kwa Pemba kutoka vituo vitano yaani Mkoani, Chake Chake, Wete, Vitongoji na Micheweni hadi kufikia vituo 22 vitakavyotoa huduma hiyo. Lengo kuu ni kuwafanya wananchi waweze kupata huduma za kinga pamoja na kujipima afya zao kabla ya kuwa karibu na maeneo yao wanayoishi, pia Wizara imekuwa ikitoa fursa ya kupima wananchi afya zao katika matukio mbali mbali. Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye ufafanuzi wa hali ya juu mno naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri kwamba hizi *Non* C*ommunicable* D*isease* (*NCD)* zinasababisha kwa kiasi kikubwa vifo katika nchi yetu, na kwa kuwa tofauti na maradhi mengine haya maradhi yasiyoambukizwa tiba yake kubwa ni pamoja na kujishughulisha na mambo ya mazoezi, kwa kuwa wananchi wengi katika nchi yetu uwezo wao ni mdogo sana wa kuweza kupata vifaa vile vya mazoezi na badala yake hujitembelea taratibu taratibu humo barabarani asubuhi, na kwa kuwa wenzetu nchi kadhaa hasa ikiwemo hii nchi jirani hapa Tanganyika wao tayari wana maeneo wameanzisha *gym* kwa vile watu wanaingia kule wanalipa pesa kidogo wanakwenda kufanya mazoezi.

(a) Kwa kuwa hapa Zanzibar hakuna hata sehemu moja inayomilikiwa na mtu binafsi au Serikali yenye *gym* na kwa kuwa vifaa ni ghali mno, ni lini Serikali itawashajihisha wafanyabiashara waweze kuanzisha hizi *gym* pamoja na Serikali yenyewe kuweza kuweka vituo vya *gym* kama ilivyo nchi kadhaa zilizoko kusini mwa

jangwa la Sahara ili tuweze kufanya mazoezi na hatimae kujipunguzia huu ugonjwa usioambukiza.

(b) Kwa kuwa enzi ya sheikh Aboud Jumbe Mwinyi pamoja na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume walikuwa wanajitahidi sana kuboresha huduma ya afya ya kutibu haya maradhi ya kuambukiza kwa mfano. Malaria kwa kuweza kupeleka dawa bure kwa mabalozi siku zile kulikuwa na mabalozi wa nyumba kumi kumi walikuwa wakipeleka bure na unapewa dawa hizi bila ya kununua. Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha yale mambo yaliyokuwa yakifanywa na Afro Shirazi siku zile chini ya uongozi wa Mzee Abeid Amani Karume na bwana Aboud Jumbe kwa kuweza kutuletea matibabu ya bure majumbani kwetu, kwa maradhi kama haya ya homa hizi, ili tuweze kupata matibabu ya bure na hatimae tupate afya njema ili tuweze kulipa kodi na ili Serikali yetu iweze kupata nguvu. Ni lini utarudia utaratibu ule.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwanza naomba nikiri kuwa nchi yetu imejaaliwa na hali ya hewa nzuri sana, mara nyingi tumegundua kwamba zile *gym* za kisasa huwa katika ambazo hali za hewa zao ni kali, kama vile zenye baridi kali watu hawawezi kutoka wakafanya mazoezi pwani na kadhalika, nchi yetu sisi imejaaliwa na rehema za Mwenyezi Mungu kuna fukwe nzuri za pwani kuna maeneo mbali mbali ambayo mtu anaweza kufanya mazoezi katika *natural environment* kuliko kule kwenye *gym* ambako miili yao inakua.

Lakini pili kuna vikundi mbali mbali ambavyo vimeanzishwa tayari vya mazoezi na nadhani kimoja Mheshimiwa Nassor Mazrui aliwahi kunialika ZAFIAZ aliwahi kunialika katika kikundi hicho yeye ni mlezi wa kikundi hicho cha ZAFIAZ, na bahati nzuri nilishiriki katika kufanya mazoezi, kuna vikundi kama vile kitambi noma na kadhalika. Lakini kitakwimu imegunduliwa kwamba mazoezi yana kinga maradhi haya yasiyoambukiza kwa asilimia 75 yaani kinga yake ya mwanzo kabisa ni mazoezi, mengine ndio hayo kupunguza mafuta, kula vyakula vya asili kama vile wali wa mtama ambao siku hizi umeachwa kabisa, na mambo mengine kama hayo.

Lakini la tatu hapo hapo Mheshimiwa naomba niseme kwamba vifaa vya mazoezi kweli ni ghali na ku- *establish* kitu kama *gym* inataka gharama kubwa sana, na wafanyabiashara wengi kweli hawajajikita katika eneo hilo la kuweka hizo *gym* za kufanyia mazoezi kwa sababu ya *investment* ama uwekezaji wake ni mkubwa, lakini *return* za *investment* zake ni ndogo kwa sababu bado wananchi hawajashajihika kwenda kwenye *gym*, ama kutumia hizo nyumba za mazoezi na badala yake wananchi wengi sana wanafanyia mazoezi yao maeneo ya Maisara, Mnazi Mmoja, pwani na katika fukwe mbali

mbali mpaka huku maeneo ya Jimbo la Kiembesamaki upande wa Buyu. Kwa hivyo wananchi watakapokuwa tayari na soko likawepo naamini wafanyabiashara watawekeza zaidi katika masuala ya *gym.*

Lakini jibu (b) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa kwamba hata sasa katika hii awamu inayoongozwa na Dk. Ali Mohammed Shein bado Wizara ya Afya kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inafanya jitihada kubwa sana kufikia kile kiwango ambacho tayari Zanzibar imeshapata jina na zawadi kubwa duniani yaani kama malaria mfano, sisi tumepata zawadi kuliko nchi yoyote duniani kufikia asilimia moja na kupungua kwa malaria ndani ya miaka kumi kufikia *percentage* hiyo kutoka asilimia 86%. Kwa hivyo *drop* ilitoka asilimia 86% mpaka kufikia asilimia 1%.

Sasa hivi changamoto kubwa iliyokuweko ni kujaribu ku-*maintain* yaani kile kiwango kisije kikapanda tena tu, tubakie hapo hapo au tushuke chini zaidi nacho kinahitaji gharama kubwa chini ya Serikali ya Dk. Ali Mohammed Shein pamoja na Serikali ya watu wa Marekani inatusaidia sana sasa hivi kwa kuleta vyandarua kusambaza dawa, na mradi ule wa malaria bado unaendelea.

Tunashukuru sana kwamba maradhi mengine yanayoambukiza kama colera, smoll pox, chicken pox, HIV AIDS, Ibolla mungu atunusuru bado hatujafikia huko, lakini maradhi mengine yote yanaambukiza naweza kusema yapo katika *control* nzuri kwa kuleta ile kinga zaidi, yaani kama maji yaliyotuwama, au maji yasichanganyike na maji yaliyokuwa na kinyesi na kadhalika. Kwa hivyo huko tunashukuru ila maradhi makuu ambayo bado yanaendelea kushughulikiwa ni Malaria, TB na HIV AIDS, juzi kwa bahati nzuri tulipata ujumbe mkubwa sana kutoka Bunge la Marekani walikuja kututembelea wao wamekuja kuhakiki vipi fedha za wachangia kodi wao zinavyotumika kupitia afya, walikuja kwa miradi mitatu tu Malaria, TB na HIV. Kwa taarifa zenu Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako Zanzibar tumepongezwa sana na tumekuwa mfano katika Afrika nzima katika kudhibiti maradhi haya matatu. Ahsante sana.

Na. 26

Hali Mbaya ya Huduma kwa Hospitali ya Kwamtipura

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza.

Hivi karibuni Serikali imekuja na mpango wa kuongeza wigo wa huduma za afya katika maeneo mbali mbali kwa kutumia vituo vya afya, hospitali na zahanati zilizomo katika maeneo hayo, kwa nia ya kupunguza msongamano

katika Hospitali ya Mnazimmoja. Hospitali ya Kwamtipura ni miongoni mwa vituo vinavyosaidia sana kupunguza msongamano wa watu katika Hospitali kuu ya Mnzimmoja, hata hivyo. Hospitali hiyo imekuwa katika hali mbaya isiyoridhisha hata kidogo kutokana na ongezeko la watu.

Je, lini Hospitali ya Kwamtipura itaimarisha huduma zake hasa ikizingatiwa kuwa huduma za macho zimehamishiwa hapo kutoka Hospitali kuu ya Mnazimmoja na ile ya KMKM.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 26 kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli Hospitali ya Kwamtipura hivi sasa imekuwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa hususan baada ya huduma za macho za Mnazimmoja kuhamishiwa katika kituo cha Kwamtipura, na hilo ni zoezi la muda tu mpaka matengenezo yatakapokamilika Hospitali ya Mnazi Mmoja huduma hizo zitarudishwa. Katika kuhakikisha kuwa kituo cha Kwamtipura kinatoa huduma katika mazingira mazuri na kwa ubora unaotakiwa, juhudi kadhaa zinaendelea kufanyika zikiwemo zifuatazo.

1) Kuongeza idadi ya Wafanyakazi wa kada zote ambapo sasa kituo hicho kinatoa huduma za afya hadi saa 3.00 Usiku.

2) Kuchimba kisima na kuweka tangi jipya na kubwa zaidi ili maji yapatikane na kuhakikisha kwamba maji yanakuwa ni mengi na yanapatikana kwa muda wote.

3) Matengenezo makubwa yamefanyika katika kituo hichi ikiwemo paa, sehemu ya maabara na sehemu ya kutoa huduma za kinamama.

4) Ujenzi wa chumba maalum kwa ajili ya huduma za mama baada ya mimba kuharibika yaani *post abortion care* ambazo zinategemewa kuanza hivi karibuni baadaya wafanyakazi kupatiwa hayo mafunzo maalum.

Mhe. Naibu Spika, juhudi hizi za kuimarisha vituo vya afya zinaendelea na pia katika vituo vya jirani vya Chumbuni, Sebleni na Mpendae ili kuongeza huduma katika maeneo hayo na kuipunguzia mzigo mkubwa ambayo hospitali ya Mnazi mmoja inabeba, na hicho kituo cha afya cha Kwamtipura kinachobeba hivi sasa kutokana na huduma za macho kuhamishiwa hapo. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwatambulishe ugeni wetu wa leo uliokuja hapa kwa ajili ya mafunzo, tunao viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Shiriki cha Elimu Chukwani, jumla yao wako 27 wanaongozwa na Rais wao Ndugu Hassan Juma, pamoja na Katibu wao Ndugu Salha Ahmed pamoja na wanafunzi wote nawashkuru karibuni sana. Ahsante kaeni.

Nina matangazo mawili Waheshimiwa tunategemea Mswada wetu tuumalize kipindi hichi cha asubuhi kwa hivyo wale Waheshimiwa waliotoka nje basi watoke mara moja warudi, ili tuje kusikiliza wachangiaji wachache waliobakia, baadaye tumuite Naibu Waziri na Waziri ili tuweze kuumaliza Mswada wetu.

Lakini nimepewa tangazo na Mheshimiwa Spika niseme kuwa Kamati ya Uongozi, Jumapili tutakutana hapa saa 4.00 asubuhi ukumbi wa juu, kuna mambo fulani ya kuyapitia. Kwa hivyo naomba aliyekuwa hayupo mkipata habari hizi mumjulishe, saa nne siku ya jumapili ukumbi wa juu wana mkutano wa uongozi kamati ya uongozi.

Mhe. Spika, aliniachia jina moja tu jana lakini bahati nzuri wameongezeka na Waheshimiwa watatu kwa hivyo tujali muda, namuanza Mheshimiwa Rufai Said Rufai, baadae afuatie Mhe. Panya Ali Abdalla, afuatie Mhe. Hassan Hamad Omar na mwisho Mheshimiwa Marina.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu Ijumaa hii tukufu kuweza kupata nafasi ya kuweza kutoa mawazo yangu katika Mswada huu wa Sheria, Sheria ya kuanzisha Shirika la Nyumba la Zanzibar ya 2014.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niishukuru sana Wizara kuliona hili ijapokuwa kwamba kiasi fulani Mswada huu umechelewa sana katika nchi yetu ya Zanzibar, na wenzetu waliouanzisha mapema faida yake naona kwamba wameshaiona kwamba kuwa na sheria hii ya Shirika la nyumba tayari wenzetu wamepiga hatua kubwa sana, ambapo sisi sasa hivi ndio tunataka kulianzisha jambo hili. Lakini juu ya hivyo niishukuru Wizara kwa kulifikisha katika chombo hiki na kutoa baraka zake ili tuweze kuwa na sheria kama hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwenye kifungu cha 7 kazi za Shirika, katika kazi za Shirika ziko kazi mbili tu nisome hii ya mwanzo. "Kazi za shirika litakuwa kuwawezesha Wazanzibari kupata nyumba na majengo mengine kwa matumizi ya makaazi, biashara, viwanda au milki ya majengo kwa vigezo shirika litakavyoamua. Hili ni jambo zuri kwa sababu tunao Wazanzibari wengi fedha wanazo lakini muda wa kusimamia masuala ya

ujenzi kwao imekuwa ni shida, imekuwa ni tabu sana, lakini toka hapo wameanzisha hili shirika na wakaanzisha jukumu hilo la ujenzi basi watawasaidia Wazanzibari wengi ambao wana hamu na wana familia zao lakini muda wa kufanya mambo hayo imekuwa ni kikwazo kwao. Kwa hivyo shirika hili litakapoanzisha mradi huu nadhani itanyanyua kipato cha shirika na kipato cha nchi yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo hili ni jambo la muhimu sana na ni jambo lenye kutiliwa tamaa kwa wananchi wetu ili iweze kupatikana.

Lakini kuanzisha maeneo ya biashara sote tunafahamu kwamba Zanzibar ni kisiwa na shughuli nyingi za Wazanzibari ni biashara, maeneo mengi sasa hivi yamekuwa ni msongamano kutokana na wafanyabiashara wanavyojikusanya makundi mbali mbali, ni kadhia biashara zao hazina ukunjufu baadhi ya maeneo mengi ndio unakuta kwamba baadhi ya maeneo ndio zinatokea ajali za mara kwa mara kutokana na wafanyabiashara walivyojikusanya kwenye maeneo madogo lakini wafanyabiashara wengi. Lakini hili shirika litakapoona hili kwamba kujenga majengo ya biashara katika maeneo mbali mbali ni njia moja wapo ambayo itawawezesha kwanza kupunguza ule msongamano, na kuwafanya watu wawe na pupa ya kukimbilia katika maeneo mengine, kwa sababu wafanyabiashara ni watu wanaoshindana kibiashara. Kwa hivyo maeneo fulani biashara hiyo inakuwa na unafuu basi wananchi wetu wengi watakimbilia katika maeneo yale ili kupata manufaa katika shughuli zao za maisha hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika kazi ya pili ya shirika ni kupangisha na kukusanya kodi kutoka kwa wapangaji na kukusanya mapato mengine kutoka vianzio vyengine vya mapato vya shirika, chini ya vifungu vya sheria hii. Mheshimiwa suala la ukusanyaji wa mapato ni *source* kubwa na hapa ndio sehemu nyeti ambayo Serikali yetu inapata usumbufu wa mapato utakapokosa usimamiaji, mara nyingi hapa Barazani ni shahidi kusikia maneno kwamba aa bwana sote ni Wazanzibari sote hapa tunaishi baba mmoja mama mmoja. Sasa tunapokuwa na mawazo haya ndio utakuta hatupigi hatua ya kwenda mbele, jambo lolote tayari lililowekewa sheria wajibu wake ni kusimamiwa sheria ile, tumesema tunajenga tukusanye mapato basi ni lazima tusimamie ukusanyaji wa mapato kama hatutosimamia basi sheria hizi zitakuwa hazina maana yoyote.

Itakuwa ni kuandika tu kupoteza karatasi na wino, lakini usimamizi wetu mbovu, maendeleo itakuwa ni vigumu kuyafikia. Kwa hivyo, suala hilo la ukusanyaji wa mapato halitaki muhali. Hili halitaki muhali, ili tuhakikishe kwamba kila aliyetakiwa, yaani kila mwenye kukodi ahakikishe ametoa kodi ili kuifanya nchi yetu ipige hatua mbele. Kinyume na hivyo, itakuwa hatufiki *millennium* tuliyoikusudia kwamba Zanzibar ifikapo 2020 iwe tayari imeshaendelea.

he. Naibu Spika, nikiacha hilo nije katika kifungu cha 7(3)(f) inasema kwamba;

" Kuendeleza nyumba na kuendeleza makaazi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi".

Mhe. Naibu Spika, katika kazi za shirika, hii kazi moja kubwa. Wote ni mashahidi kwamba tunao majumba humu hayapo rasmi, mengine ni magofu, mengine yapo katika hali mbaya, lakini baadhi ya mengine yapo katika hali mbaya, lakini wananchi wetu bado wanaishi katika majumba hayo. Kwa hivyo, naliomba sana shirika litakapoanzisha kuanza hizi kazi zake, basi zile nyumba ambazo hazipo rasmi wazione haraka ili waje kuziafu roho za wananchi wetu ambao bado wanaishi katika majumba hayo, ili ziwe ni nyumba zenye kiwango inayoweza kuishi mwanadamu akawa hana wasi wasi usiku, wala hana wasi wasi mchana wakati upepo unapotokea.

Mhe. Naibu Spika, kazi hii ni kazi ambayo inahitaji mapesa, kuliondosha jengo katika hali yake iliyo ya ubovu na kulipeleka katika hali ni nzuri, panahitaji mapesa. Kwa hivyo, kama tutakosa usimamiaji basi kazi hiyo hatutoweza kuifikia. Kwa hivyo, naomba sana mimi masuala ya usimamiaji tuyape kipa umbele ili kuweze kufikia malengo tuliyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika Sehemu ya Tatu, Utawala na Uongozi wa Shirika. Kuna sifa pale za Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi. Sifa ya kwanza katika kifungu cha 9 inasema kwamba;

Kifungu cha 9(1) "Katika uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, kutazingatiwa ufahamu, taaluma, uzoefu na uelewa katika mambo yanayohusiana na utawala au makaazi".

Mhe. Naibu Spika, hizi sifa sio mbaya, lakini katika hii sifa moja ambayo mimi naona haikunikalia vizuri sikupata ufafanuzi nalo ni suala la taaluma. Katika kumtafuta Mwenyekiti wa Bodi inawezekana Mwenyekiti huyu ana taaluma mbali mbali, lakini taaluma ya ujenzi hana. Lakini ni mwingi wa taaluma, lakini kazi tunayoitaka ni mtu mwenye sifa hii. Kwa hivyo, hii taama ilikuwa ielezwe taaluma gani Mwenyekiti wa Bodi anaetakiwa hapa. Kwanza iwe ile ambayo tunayoihitaji, halafu zifuatie taaluma nyengine.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. waziri, Waheshimiwa Wajumbe, waliopita jana hapa baadhi yao walimuharakisha asije akachelewesha Kanuni. Hii Kanuni ni muhimu katika kazi hii, kama ilivyoagiza hii sheria. Mimi nashukuru sana sheria ya mara hii imeweka ufafanuzi kwa masuala ya Mhe. Waziri katika kupatikana Kanuni.

Mara nyingi tunapotunga sheria hizi za Kanuni huambiwa tu waziri atatayarisha Kanuni, anaweza kutayarisha Kanuni. Lakini mara hii imeeleza wazi kwamba Waziri atatengeneza haikumpa ile kutengeneza au kutokutengeneza haikumpa muda, haikumpa kushauri kwamba afanye au asifanye, imemtaka afanye. Kwa hivyo, fursa hii aliyoipata waziri basi aitumilie ili shirika hili liweze kwenda vizuri na kuweza kuifafanua sheria ili kwa yoyote yule atakaepata majukumu haya aweze kufanya kazi yake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, kupata taaluma ambayo inahusu na lile jambo linaloombewa, hili ni jambo la umuhimu sana. Kwa sababu Mwenyekiti huyu atakuwa anafahamu kile ambacho ameteuliwa na anachokifanyiwa kazi. Lakini isiwe kwa Mwenyekiti tu na hawa baadhi ya Wajumbe ambao wataungana na Mwenyekiti, sifa hizi wawe wanazo. Isije wakateuliwa watu ambao hawana sifa ya ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije katika kifungu cha 27, hapa kuna upangaji wa kodi. Katika upangaji wa kodi katika kifungu cha (2) kimefafanunua namna ya majengo yenyewe yalivyo. Katika upangaji wa kodi chini ya kifungu hiki, shirika litazingatia yafuatayo, kuna karibuni mambo matano, ukubwa wa jengo, hilo ni jambo zuri. Kodi iangaliwe jinsi ya jengo lenyewe lilivyo, isiwe kodi yote ipo ya aina moja. Hapa nashukuru sana wanasheria wameona jambo la maana sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, kuna matumizi ya jengo. Matumizi kuna matumizi ya aina mbali mbali, kuna wengine wanaweka viwanda, mambo mbali mbali. Kwa hivyo, kutokana na zile harakati ya lile jengo linavyotumiwa basi na ile kodi iende kutokana na jengo halisi lilivyo, lakini pia, kuna thamani ya jengo.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika haya majengo tuliyonayo ya Serikali asilimia ya wananchi wanaopangisha mule ni vijana wetu, watoto wa wakulima na wakwezi kwa asilimia kubwa. Katika asilimia hiyo wengi wao ndio masikini, wengine wanatimiza miaka miwili, mitatu hawajalipa kodi. Hawajalipa sio kwa sababu hawataki, hapana. Hawajalipa kutokana na uwezo wao. Watu hawa mimi nahisi kama walivyosema baadhi hapa jana kwamba, baada ya sheria hii kupita, lazima shirika litaangalia namna gani wanzishe kodi mpya.

Lakini katika kuanzisha kwa kodi hizi, ni lazima waangaliwe wanyonge wa Zanzibar wanaoishi katika majengo yale. Baadhi yao hawatimizi hata mlo, wanaishi katika majengo yale. Kwa hiyo, lazima shirika liwaangalie sana masikini hawa. Ukisema huyu umtoe katika jengo lile utampeleka wapi?

Itakuwa ni dhiki. Kwa hivyo, ni lazima watu hawa waangaliwe na kodi zao zisilingane na wale ambao kidogo wana uwezo kiasi fulani.

Mhe. Naibu Spika, katika haya majengo kuna baadhi ya majengo haya yako mjini. Ukitizama eneo ni zuri, jengo liko mjini mahali pazuri, lakini udhaifu wa jengo mengine mabovu kabisa. Kwa hivyo, katika kupanga hizi kodi pasije pakaangaliwa tu kwamba ah! Jengo hili wakati lipo mjini, bei yake mpangaji atatakiwa alipe bei fulani, hapa tutakuja kuwakwaza.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema shirika litembelee majengo yake, ione hali halisi ya majengo yalivyo, hata ikiwa lipo mjini, lakini linaweza kushindwa thamani na jengo ambalo lipo ng'ambo ya mji kutokana na hali ya jengo lilivyo. Kwa hivyo, pasijepakatolewa maamuzi tu wakati hili jengo lipo mjini, bei yake itakuwa ya kimjini mjini, lakini uhalisia wa jengo halipo katika hali nzuri. Kwa hivyo, ningeliomba sana watu wa shirika hilo waje walione sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia niseme kwamba kuna kifungu cha 29 kuhusu Malipo ya Kodi. Katika malipo ya kodi sheria hapa inasema kwamba mkodiji yeyote yule atalipa kodi yake mwanzo wa mwezi, watakapokubaliana na shirika.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nimepata utata kidogo kwamba baadhi ya watu wanaoishi katika majumba ya kukodi, baadhi yao ni wafanyakazi, wengine wanafanya kazi katika mataasisi mbali mbali ya Serikali na ya watu binafsi. Lakini katika utaratibu wa malipo ya wafanyakazi wetu mara nyingi huwa yanaanza kuanzia tarehe 21 hadi mwisho wa mwezi pengine hata mwezi unaofuatia watu hawa wakawa hawajapata malipo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, sheria inavyosema kwamba mwisho wa mwezi, yaani mwanzo wa mwezi mtu alipe kodi yake. Hapa kiasi fulani tutakuja kuwakwaza wananchi wetu wanaofanya kazi katika maidara ya mashirika mbali mbali na ya watu binafsi kwamba mwanzo wa mwezi akawa pesa ile hajaitia mkononi. Lakini na malengo yake ni kulipa na kama hakulipa amewekewa faini. Sasa hilo litakuwa ni tatizo, ni vyema Mhe. waziri, atakapotunga Kanuni zake katika suala hili la malipo basi aliweke katika mustakbali ambao wananchi wetu hatutopata dhiki juu ya ulipaji huu wa kodi katika yale maeneo ambayo wameyakodi.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante na wewe tunakushukuru, sasa nafasi ya Mhe. bi Panya Ali Abdalla na baadae afuatie Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote na mimi sina budi na nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai, kuweza kukutana hapa asubuhi hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ili niweze kusema machache juu ya mswada huu. Pia, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote, niwapongeze kwa dhati kwa jinsi ambavyo wamefanikiwa kutayarisha mswada huu na wakauleta katika wakati muwafaka.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mswada huu sina mengi ya kusema kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati tumeupitia mswada huu kifungu kwa kifungu na tukaboresha tuliyoboresha. Tangu tumeanza tangu waziri na Mwenyekiti waliposoma ripoti hii Wajumbe wameichangia kwa kina na kuiboresha, kubwa nilisema mimi labda kama itakuwa si busara kama Mjumbe wa Kamati ili na mimi nioneshe kwamba nauunga mkono kwa dhati mswada huu uweze kufanikiwa kupita. Kwani naelewa mswada huu utakapopita basi mafanikio makubwa yataweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, mimi niungane na Wajumbe waliopita niseme kwamba mswada huu au nichukue fursa hii kuwashawishi sana Wajumbe wenzangu tuweze kuunga mkono mswada huu kwa lengo la kuelewa kwamba mswada huu utakapopita basi ni mafanikio makubwa yataweza kupatikana katika nchi yetu na tutaweza kufaidika Wazanzibari na vizazi vyetu. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuwashawishi Wajumbe wenzangu ili tuupitishe mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba wizara imejipanga juu ya hili. Kwa sababu sisi tukiwa ni Wajumbe wa Kamati kuna Wajumbe wenzangu walipokuwa wakichangia jana walisema je, kuna wigo wowote labda tumeweza kukopiya mahali. Mimi naamini kwa kuwa jambo hili ni kubwa ambalo wanataka kulianzisha basi naamini wizara imejipanga na imekopia. Mimi kama ni Mjumbe wa Kamati nitasema kwamba tulikwenda kujifunza kwa wenzetu hapo Bara. Kwa hiyo, naamimi na wao wamechukua juhudi mbali mbali za kuweza kutafuta hapa na pale ili waweze kuona kitu hicho wanachokianzisha hakikwami na kinafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme mswada huu au sheria hii itakapopita basi shirika naamini litaweza kufanya vizuri hasa litakapopata nyenzo ya kuweza kuanzisha mpango ambao wamekusudia kutaka kuuanzisha wa kujenga nyumba. Basi naamini kisiwa chetu hichi kitakuwa katika hali nzuri, hali ya kupendeza. Hali ambayo itaweza basi kuleta ile dhana nzima ya muasisi wetu marehemu Karume ambayo aliianzisha kwa ubunifu wake tangu hapo awali,

kwa sababu yeye alikuwa ni mbunifu na akiwapenda raia wake wakae katika maisha bora.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme katika shirika hili wenzangu wamechangia mambo mengi katika huu mswada. Mimi nilikuwa naona kuna kifungu hichi cha 49(2) ambacho kinasema;

"Endapo amri au maelekezo husika yametangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali, watu wote watakuwa wanayo taarifa hiyo".

Mhe. Naibu Spika, hapa tu mimi niongeze neno, kwa sababu si rahisi kama tangazo au gazeti linapotoka au matangazo mbali mbali kutumia vyombo vyetu labda watu wote wakaweza kupata habari. Inawezekana wengine wasiweze kupata, labda hapa tuongeze neno kwamba taarifa hizi kama kuna watu maalum kwamba tunataka kuwapelekea basi ni vizuri, hata kutumia barua kwa kuona taarifa hii mtu inamfika rasmi. Kwa sababu tunaweza kusema kwamba ameshasikia tangazo na akaja kukumbana na adhabu huko kumbe pengine yeye hakuweza kusikia.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kweli nilisema sina mazungumzo mengi juu ya hili. Lakini niendelee kusema tuupitishe mswada huu kwani faida nyingi zinaweza kupatikana kwa kupitisha mswada huu. Wananchi wetu wataweza kupata makaazi bora, lakini pia, mji wetu unaweza kupendeza kuwa katika hali nzuri. Vile vile, shirika linaweza likajipatia uwezo mkubwa tu wa kuzalisha na nchi yetu ikakuwa kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nisisitize wenzangu walieleza kuhusu mipango miji ambapo shirika hili litapoanza kazi zake basi ni vizuri kuzingatia huo mpango. Mimi nasisitiza hasa katika maeneo ya mjini ambapo ni sehemu kubwa sana ambapo ndio kimbilio la wananchi katika harakati zao za kazi, basi pia kuzingatia suala zima la *packing* za magari. Kwani tunaona hivi sasa tu watu wanavyohangaika katika ku-*pack* magari wakati hata bado hatujafikia huko mbele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nasisitiza hiyo *packing* ya magari ni muhimu, kwani hata tulipotembelea pale Dar-es-Salaam tuliona nyumba nyengine ambazo wameshajenga za ghorofa wananchi tu wenyewe kwa kutaka kuona wanajenga majengo mazuri, lakini wakakosa kuweka *packing*, yaani suala hilo wakalisahau. Kwa hiyo, tumeona *packing* za magari unaweza kuzunguka kutwa nzima hujapata sehemu ya ku-*pack*. Lakini kwa wale ambao tayari watu wa shirika wameanzisha basi hili wameliona na wakalipa kipaumbele na wakaweza kulishughulikia.

Tumeona majengo ambayo wao wameyashughulikia hili wamelizingatia, kwa hiyo, na mimi nasisitiza tutakapoanzisha shirika letu hapa tuhakikishe *packing* za magari, ni kitu muhimu, kwa sababu mji wetu unakuwa na maendeleo yanakuwa, vyombo vinakuwa vingi, kwa hiyo, tuweze kulishughulikia kwa dhati suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi ya kusemam isipokuwa mimi mwenyewe kwa niaba yangu na wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Pia, nachukua fursa hii kuwashawishi Wajumbe wenzangu tuunge mkono mswada huu ili upite na shirika liweze kupata nafasi ya kuweza kufanya kazi zake. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa na wewe, kaongezeka mchangiaji mwengine, kwa hiyo, tunamalizia sasa hivi Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Marina na baadae Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana llahu Wataala* aliotujaalia kuwa katika uhai, uzima na afya imeturuhusu, pamoja na wenzangu wote tuliohudhuria katika Baraza lako hili tukufu kwa mujibu wa kazi zetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kukushukuru na wewe uliyenipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu katika mswada huu wa uanzishaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar. Vile vile, nimpongeze sana Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote kwa kutuletea mswada huu kipindi muafaka, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awape uwezo ili waweze kukidhi haja kwa yale aliyokusudia kuyafanya.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, katika utangulizi wangu niseme tu Mwenyezi Mungu *Subhanahu llahu Wataala* aliumba ardhi kwanza kabla ya kumuumba mwanadamu lengo kuu la uwepo wa ardhi ni kuishi viumbe wanaadamu, wanyama hata na majini. Lakini na mambo mengineyo tukitafuta rizki kwa ajili ya kuendesha maisha.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na utangulizi wangu ukizingatia hayo utakuta mambo mengi yafuatayo:uwepo wa ardhi, uwepo wa watu, uongozi bora na unaozingatia maadili ya utu wa mwanaadamu.

Mhe. Naibu Spika, kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba Zanzibar ni jambo zuri. Mimi nimepata fursa Kamati ya Mawasiliano na Majenzi iliyopita na hata iliyopo kwa mujibu wa mchangiaji aliyepita. Tulitembelea Dar es Salaam na maeneo mbali mbali tukakuta Shirika la Nyumba la Kitaifa limepiga hatua kubwa sana ambao shirika lile halijiendeshi kihasara, linajiendesha kwa faida

kubwa sana. Zile takwimu zimenipita walivyotwambia pesa waliyonayo lakini pesa nyingi sana. Sasa na sisi kuelekea huko shirika lisije likaendesha shughuli zake kwa hasara, shirika liwepo kwa kufika maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na mchango wangu katika kifungu cha 3(2) naomba kwa ruhusa yako ninukuu:

"Shirika litakuwa ni chombo kinachojitegemea cha kudumu chenye muhuri wake na kwa kutumia jina lake litakalokuwa na uwezo:

(a) Kupata na kuchukua au kutoa mali anayoimiliki inayohamishika au isiyohamishika;

(b) Kuingia katika mkataba na mtu yoyote na Taasisi;

(c) Kushtaki na kushtakiwa;

(d) Kukopa na kukopesha fedha; na

(e) Kushiriki kufanya shughuli zozote kwa mujibu wa sheria ambazo zinaweza kufanywa na chombo chochote chenye hadhi ya shirika".

Mhe. Naibu Spika, tukizingatia hilo shirika kufikia malengo hayo lazima shirika lifuate Sera ya Ardhi upande wa dhamira ambayo ni kutumia ardhi ya Zanzibar kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Lengo kubwa ya kuitumia ardhi ya Zanzibar kwa kuleta maendeleo ya kijamii na baadae ya kiuchumi, kwa hivyo, wananchi hapa wamepewa kipaumbele sana katika kuitumia hii ardhi. Kwa hivyo, ikiwa tutafuata Sera hii ya Ardhi, basi shirika litapata mafanikio makubwa sana na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu katika kuendeleza shughuli hii ya Shirika la Nyumba kuanzishwe miji mipya kwa kujenga majumba ya ghorofa kwa sababu sisi na wenzetu kule ni tofauti sana. Ardhi yetu sisi ni ndogo na finyu kabisa ukilinganisha na wenzetu wa Tanzania Bara. Tanzania Bara pamoja na majengo yote yale, lakini unakwenda kilomita nyingi bado pori lipo, lakini hapa unaweza kuzunguka kisiwa kwa siku moja tu. Kwa hivyo, kama tutafuata sera yao ya ardhi itafika kuleta mambo yaliyo mazuri na kupata mafanikio.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kutengwe maeneo mapya kwa ajili ya kutanua miundombinu ya kiuchumi wakati wa shughuli za ujenzi wa majumba. Maana katika shughuli hizi za majumba lazima iwepo miundombinu ukija na baadae kutegemea na hii ardhi yetu ilivyo ndogo sio leo umejenga nyumba kesho

ukaambiwa vunja si malengo mazuri wala hayana mafanikio. Kwa hivyo, tujenge nyumba madhubuti na kutanua miundombinu yetu kuwa mizuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuwepo fursa sawa baina ya masikini na matajiri kwa sababu tunaweza kuwa na dhamira hizi nzuri, lakini hatima yake baada ya shirika kujenga nyumba ikawa yule maskini hafaidiki na chochote, hili ni tatizo. Kwa hivyo, maskini na yeye apewe kipaumbele cha kuishi vizuri kama mwanaadam ndio jambo hili litakuwa na mafanikio mazuri kama ilivyokusudiwa, mwenyewe alikuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar (Marehemu mzee Abeid Amani Karume) kwamba kila mtu aishi vizuri hatukufikia malengo. Lakini ukiangalia utakuta wale matajiri ndio wanaopewa kipaumbele, lakini maskini ya Mungu hapati chochote, utamtoa katika umaskini lini kila siku unamdumaza? Hili si jambo zuri.

Vile vile, kusiwepo na upendeleo katika ugawaji wa ardhi, kwa sababu kila mtu anayo haki ya kupata sehemu yake kwa mujibu wa utaratibu wa sheria tulizojiwekea. Lakini ukifanya upendeleo basi inakuwa wengine hawafikii hayo malengo ila hubakia na matatizo.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika uendeshaji uwezo na utaratibu katika ukurasa wa 13 kifungu cha 24, 25 na 26 yameelezwa mambo mengi mazuri na hatua za mikakati zitakazosimamiwa na shirika. Katika vifungu hivyo nilivyovitaja sitanukuu, lakini kuna mambo mazuri tu yaliyoelezwa katika mambo ya mkakati na shughuli zilivyosimamiwa na shirika.

Mhe. Naibu Spika, shirika kama litasimamia vizuri malengo yake iliyojiwekea basi Zanzibar itapiga hatua nzuri katika mambo ya majenzi yaliyokusudiwa. Tuangalie changamoto za ushirika mbali mbali zilizojitokeza katika mashirika kadhaa yaliyokuwepo hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tatizo sio shirika, isipokuwa ni usimamizi mzuri kwa sababu kama ni mashirika tunayo mengi, lakini usimamizi unakuwa si mzuri. Kwa mfano tunalo Shirika la Usafiri wa baharini, haya tuone leo Shirika la Meli hali inavyokuwa mpaka unahakikisha meli ishazeeka ndio inatafutwa nyengine, huku ni kulidumaza shirika wala hukuti mtu yoyote kuulizwa kwa nini shirika hili limepoteza malengo yake au kufa kabisa hatujawi kuona. Mtu anamiki shirika kama lake, hili ni tatizo. Kama ni malengo haya kila siku tutatunga sheria hapa na hazina mafanikio.

Tulikuwa na shirika la magari hapa lilikuwa linafanya kazi zake Unguja na Pemba, ilikuwa tunaona mabasi jinsi yanavyofanya kazi, liko wapi? Ni matatizo tu. Tulikuwa na shirika la uvuvi, yako wapi maboti yale? Yako Maruhubi juu yamekwezwa, hakuna kinachofanyika, haya sisi kila siku

tutakuwa tunaounda mashirika hatima yake hatupati hayo maendeleo tuliyokusudia. Ni tatizo sana.

Mhe. Naibu Spika, shirika la viwanda vidogo vidogo Amani huko yote yamepoteza mwelekeo, sasa Waheshimiwa kama nilivyoeleza mwanzo kule kama wenzetu Tanzania Bara wamepiga hatua. Shirika la Nyumba la Taifa kila sehemu liko, wamejenga nyumba kubwa, wamejenga nyumba ndogo ndogo. Tulikwenda sehemu ya Kigamboni wakatupeleka Idara ya Nyumba Zanzibar, waliwahi kutupeleka kule, tumekuta nyumba wanajenga, kabla ya kumalizika kujenga nyumba zote zimeshamalizika watu washalipa kodi zao mtu anakuja kumaliza nyumba tayari kwa kukabidhiwa tu. Miundombinu yote ipo kama umeme, maji na kila kitu, ni mashahidi hawa, Mkurugenzi wa Idara ya Nyumba ni shahidi kwa sababu tulikwenda wote.

Sasa na wao wajifunze kutokana na yale tuliyokwenda yakuta bila ya hivyo itakuwa hatufiki na mashirika mengi yamekufa kutokana na ukosefu wa uadilifu. Kama tungekuwa waadilifu basi mashirika yetu yangeendelea, lakini kama alivyozungumza unamuweka mtu katika shirika analimiliki kama la kwake.

Mhe. Spika, mimi naomba mchango wangu mdogo uishio hapo, lakini wazingatie sana haya tuliyoyaeleza, wakiyazingatia haya watapata mafanikio makubwa. Ninakushukuru sana kwa mchango wangu huo.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante, Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba Zanzibar. Naomba niipongeze Serikali kwa kukubali kuuleta mswada huu mbele ya Baraza lako Tukufu kuujadili na hatimaye kuupitisha ili uweze kutekelezeka katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia, nampongeza waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi hii nzuri ambayo wanayoifanya siku hadi siku. Mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hii. Tumeupitia mswada huu kwa kina tumeufanyia marekebisho mbali mbali, maboresho ya vifungu mbali mbali vya mswada huu na hata katika taarifa ya Kamati imeeleza baadhi ya maboresho hayo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu wa kuanzishwa Shirika la Nyumba Zanzibar ni mzuri na nasema hivyo kwa sababu kwanza kitakuwa ni chombo ambacho kimeanzishwa kisheria. Pili, kitakuwa na mamlaka ya kupanga kodi zake kama itakavyoona inafaa na pia, kitakuwa na uwezo wa kujenga nyumba, kukodisha, kuuza kwa mujibu wa mahitaji itakavyohitajika na kitakuwa na uwezo wa kuzifanyia matengenezo endelevu nyumba mbali mbali ambazo wanazimiliki shirika hili.

Mhe. Naibu Spika, pia, shirika litakuwa na uwezo wa kupata mikopo kutoka taasisi mbali mbali za kifedha. Kwa hivyo, wakipata mikopo ina maana litakuwa na uwezo wa kujenga nyumba nyingi zaidi na litakuwa na uwezo wa kufanya miradi mbali mbali ya maendeleo ambayo itawasaidia wananchi wetu na nchi kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia mfano wa wenzetu hapa Shirika la Nyumba la Tanzania wamepiga hatua kubwa sana na ili shirika hili lijiendeshe hawa watendaji wetu ambao watakaofanya kazi katika shirika hili wapatiwe taaluma kujifunza zaidi ili watakavyoanza kufanya kazi hizi katika shirika wafanye kazi kwa uadilifu na hatimaye kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuiga mazuri si dhambi; mazuri yanaigwa tu madhali yanaendeleza nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, pia, ningemshauri Mhe. waziri, kuhusu shirika hili litakapoanzishwa wajaribu kutafuta wataalamu wenye uwezo, ujuzi, uzoefu na uzalendo, tusitafute watu ambao alimradi tumuweke, lakini tukifanya hivyo kuwatafuta watu ambao hawana uzoefu, hawana ujuzi, hawana utaalamu katika fani mbali mbali ambazo shirika litahitaji, tunaweza tukalipeleka shirika pabaya. Kwa hivyo, tutafute wataalamu wenye uwezo, uzoefu na taaluma ambazo shirika zinahitaji katika kufanya kazi zake siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja nataka ufafanuzi kwa Mhe. waziri, kuna suala zima hili la Mji Mkongwe ambalo kuna baadhi ya nyumba za Mji Mkongwe nyingi zimechakaa na nyengine hatimaye kuanguka na ukiangalia Mji Mkongwe nako kuna mikataba mbali mbali ya kuhifadhi Mji Mkongwe, hasa tukianzisha hili shirika la nyumba na ujenzi wake utakuwa si chini ya ghorofa pengine 10, 15, 20 na ukiangalia katika mikataba ya Kimataifa kama *UNESCO* pengine ninavyoelewa na kama nimekosea Mhe. waziri, naomba unikosoe, wanajenga nyumba ghorofa si zaidi ya ghorofa tatu.

Sasa kutokana na kuanzishwa shirika hili ambapo linaweza likajenga zaidi ya ghorofa 10 au 15 hapa, nilikuwa naomba maelezo tu kwa Mhe. waziri, vipi katika maeneo ya Mji Mkongwe hali hiyo itakuwaje? Kwa sababu majengo yako mengi machakavu na mengine yamebomoka na kutokana na mikataba mbali mbali ya *UNESCO* uhifadhi wa Mji Mkongwe yameweka mikakati pengine labda ijengwe nyumba kama ghorofa tatu, nne lakini si zaidi ya ghorofa, wenzetu Tanzania Bara wanajenga ghorofa 10, 15 na 20.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi ya kusema ila ninasimma hapa kuunga mkono mswada huu na naomba Wajumbe wenzangu waunge mkono ili tuendeleze Taifa letu. Ahsante.

Mhe. Hussein Ibarahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu kuwa wote katika afya njema na salama kabisa. Pia, nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii kuwa ni mchangiaji wa mwisho kabisa kwa siku ya leo. Lakini pia, nimpongeze sana Mhe. waziri, kwa juhudi yake kubwa na watendaji wake kwa mswada huu. Nimpongeze Mhe. waziri, kwa umakini wake na ujasiri wake kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, lakini juzi katika Kamati yetu alipewa mamlaka Mhe. Waziri ya kuamu kitu au kuwa na majukumu, lakini yeye alikataa alisema maamuzi haya yapelekwe kwa Bodi na Bodi iweze kuamua, mimi ninampongeza sana kwa umakini wa kukataa ile kazi aliyopewa kuamua yeye kasema ipelekwe kwenye Bodi.

Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. waziri, na naamini ana nia njema kabisa na nchi hii bila ya kutaka yale matakwa kwa maslahi yake au kwa ukubwa wake.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, mimi ninampongeza Mhe. waziri, kwa kutuletea mswada huu wa Shirika la Nyumba kwa kazi yake kubwa aliyoifanya mpaka mswada huu leo umefika hapa Barazani, mimi ninampongeza sana kwa nia yake njema kabisa.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, niipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia yake njema kabisa kwamba mswada huu kuutayarisha na kufika hapa, ujumla Serikali yetu wameona mswada huu ni muhimu sana ili uweze kutuletea maendeleo katika nchi yetu na kwa wananchi wanyonge ambao waliokuwa hawana nyumba waweze kumiliki nyumba kwa bei nafuu na mikopo.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuanzishwa shirika la nyumba lengo kuu ni miongoni mwa majukumu yake kuhakikisha kuwa wananchi wa visiwa hivi vya Zanzibar wanapata makaazi bora yanayoweza kuyamudu na yaliyo salama.

Mhe. Naibu Spika, na pia, mswada huu unagusa asilimia mia kwa mia wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze hapa kwenye ukurasa wa 9 (3) (e) kuhusu Shirika la Nyumba Zanzibar kushirikiana na wawekezaji wanaofaa katika ujenzi wa nyumba za kuishi watu na kwa ajili ya biashara na kukopesha watu.

Lakini mimi niseme Mjumbe mwenzangu alisema Mji Mkongwe kuna matatizo hasa katika huu uhifadhi wa Makumbusho ya Kale haya *UNESCO*, kuna sheria nyingi zimewekwa pale na ukitizama mfano mzuri hoteli iliyojengwa pale ile *HAYAT* walitaka kwenda ghorofa 10, lakini leo wameambiwa wajenge ghorofa tatu. Kwa kweli uwekezaji ule wale wanakuwa mwisho wa siku watakuwa wako katika hasara.

Ukitizama jambo la pili, soko la Malindi lile lilikuwa lijengwe vizuri na kubwa kabisa, lakini Mamlaka ya Mji Mkongwe sheria nyingi zimewekwa pale, lile soko limejengwa dogo kwa kazi kubwa mpaka ikafanikishwa kujengwa soko, lakini soko ilikuwa hawataki lijengwe pale. Kwa hiyo, naomba sana na tunapokwenda kwenye shirika la nyumba hawa jamaa wataelekeza kwenye malengo yao makubwa kwenye biashara. Kwa hivyo, naomba mkataba wa umoja huu wa *UNESCO* uangaliwe tena kwa sababu tukisema tunasubiri wao, haya maendeleo hayatofikia malengo yetu.

Mimi niseme kwenye mswada huu naupongeza sana mswada mzuri na mimi ni Mjumbe wa Kamati sina tatizo nao. Lakini kwenye ukurasa wa 13, 24 (b), wasi wasi mkubwa hapa ni huu uwezo wa kukopa kwa shirika la nyumba, tusije tukawapa uwezo wa kukopa hawa shirika la nyumba fedha benki na wakapewa pesa wakajenga majumba, lakini wakapewa sheria za kujenga nyumba ndogo ndogo.

Hawa Shirika la Nyumba watafilisika na hawatoendelea, lazima tuangalie uwezo tunaowapa na tuangalie sana eneo zuri kabisa la kujenga nyumba hasa kama Mji Mkongwe kuna maeneo mazuri pale, ukitizama Dar es Salaam wenzetu hawa wa shirika la nyumba walipotualika kwenda kujifunza sisi tumeenda, walitupeleka kwenye nyumba za maendeleo, nyumba ilikuwa karibu na bahari *Sea view*, ile bei yake inakuwa ghali na watu wengi wanapendelea kununua. Sasa kwa eneo la Forodhani pale ukijenga nyumba zile za ghorofa pale tutapata fedha nyingi na shirika nina uhakika litakuwa na uwezo wa kujiendesha na kupata pesa nyingi sana. Sasa tunawapa uwezo wa kukopa hawa shirika la nyumba wasije wakapata hasara kwa sheria hizi, naomba tuwaangalie sana.

Mhe. Naibu Spika, juzi tulikwenda China naweza kusema tulikuwa na Wajumbe baadhi baadhi nyumba tano walizojenga wenzetu wa China wakijenga pale Mji Mkongwe nyumba zote zitavunjwa zile na hazina haja kujengwa tena nyumba za chini kama vile. Nyumba tano tu tulifanya hesabu na Mhe. Abubakari, alikuwepo, lakini kama tutawazuia hawa jamaa kuwaekea sheria nyingi, hawa jamaa watakula hasara na watakula hasara na hata mikopo yao itakuwa…

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Marina, alisema hapa Mji Mkongwe kuna nyumba 13 za idara ya nyumba, ni mbovu na hawana uwezo hata wa kutengeneza nyumba hizi, zitaanguka kwa sababu zile hali zao ni mbaya ukitizama hata kodi inayolipwa na wananchi wale ni pesa kidogo. Kwa hivyo, hawana uwezo wa kuzilipia nyumba zile na kuzirekebisha, kwa hivyo, zinakwenda tu.
Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, mimi naomba sana tuangalie suala hili hawa jamaa wanapojenga haya majumba, watakopa fedha na isipokuwa nyumba ghorofa 20, hapo ndio wakaweza kufaidika wao na wakaweza kupata manufaa zaidi.

Lakini tukitizama, mimi nilikwenda Dar es Salaam kujifunza, kuna nyumba pale wamejenga *National House* wametuonesha mchikichi pale nyumba zote zimeshauzwa wamejenga ghorofa tatu juzi juzi, lakini leo nyumba moja ukitaka kwa shilingi milioni mia mbili, lakini kwa mkopo nafuu unachukua benki, unalipa kidogo kidogo nyumba hiyo inakuwa yako baada ya miaka mitano au 10, lakini unakuta mtu ana nyumba yake anamiliki kwa muda mfupi tu haraka sana. Kwa hiyo, mimi naona hili shirika la nyumba likianzishwa litatusaidia sana kwa wananchi wetu wanyonge ili waweze kufikia malengo.

Mhe. Naibu Spika, pia, tulikwenda Kigamboni kuna miradi pale wamejenga *National House* wametuonesha nyumba nafuu tu, nyumba moja ni milioni 50 inafika na uwezo ule wametupa utaalamu wa kujenga nyumba zile. Wametufahamisha nyumba hii itagharimu milioni 50 mpaka 52 kwa mkopo unaomkopesha mwananchi na anaweza kumudu nyumba ile kwa kununua. Kwa hivyo, na sisi tutaweza kujimudu kwa kupitia shirika la nyumba ili kujifunza kwa wenzetu kutufundisha utaalamu ule tuweze kujenga nyumba zile za bei nafuu kabisa kwa wananchi wetu wa Zanzibar wengi ambao hawana nyumba.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme jengine hapa Dar es Salaam ukitizama kuna nyumba imejengwa ile Machinga *Complex* lile jumba limejengwa, lakini ukitizama lile jumba ni hasara, sasa hivi watu wanauza biashara, lakini pesa zimepotea nyingi za Serikali, lakini ile nyumba haina tija yoyote kwa Serikali wala kwa wananchi kwani wananchi wanakaa, lakini kodi hawalipi. Mchikichi pale kuna nyumba ni Machinga *Complex,* kwa hiyo, naomba sana shirika la nyumba na wao wanapojenga nyumba hizi waangalie *location*, waangalie sehemu gani nzuri. Jana Mjumbe mmoja alisema vizuri sana Mhe. Hamad Masoud, alizungumza lazima kuwe na utaalamu wa kujenga hizi nyumba na kuangalia, *otherwise,* itakuwa fedha hizo watakazokopa hao wenzetu zitakuja kwenda hazina tija yoyote.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi niwapongeze sana idara yetu ya nyumba hawa ndugu zetu wameweza kukusanya karibu milioni 93 kwa kodi zetu zilizokuwa sasa hivi. Mimi nawapongeza sana kwa juhudi zao kubwa hizo, mfano pesa hizi walizokusanya milioni 93 haziwezi hata kufanya marekebisho nyumba nyingine. Tulisema mfano mdogo tu tulikwenda Pemba kwenye Kamati, nyumba ya Kengeja ile pale inaanguka sasa hivi imeshakuwa mbovu, wananchi masikini hawana uwezo wa kuhama kwenda sehemu nyingine, nyumba zao zilivunjwa kwa ajili ya nyumba zile.

Lakini idara ya nyumba haina fedha ya kuzilipia nyumba wala kutengeneza itakuwa ni bilioni 1.2. Kwa hiyo, naomba hili suala ni zuri na hao wenzetu wana nia njema kabisa kuboresha suala hili shirika la nyumba wametuchukua mara mbili kutufunza Dar es Salaam wametuonesha, mimi nampongeza sana ndugu yangu Mkurugenzi wa Idara ya Nyumba ana moyo wa uzalendo kabisa.

Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba sana Mhe. Rais, kama atateua mkurugenzi mkuu, basi ampe huyu Mwinyigogo, naomba sana bila ya kuangalia vigezo vyake na elimu yake, lakini huyu jamaa ana moyo mzuri na anajitihada na anaipenda nchi yake kwa ajili ya kazi hii anayoifanya Mheshimiwa. Kwa hiyo, naomba tumuangalie sana ndugu yetu huyu kwa jitihada yake kubwa na uzalendo wake wa nchi hii anayoipenda kabisa ili kujenga makaazi bora kwa wananchi.

Pia, nimpongeze sana Mheshimiwa, nimeangalia katika ripoti zangu za Kamati mbali mbali wameweza kufanya marekebisho nyumba za Mchina kama mabomba na mashimo ya maji machafu wameweza kufanya hawa ndugu zetu kwa juhudi zao japo fedha kidogo, lakini wameweza kufanya vitu kama hivyo. Tukitizama hapa nyumba za maendeleo hizi za Michenzani wamebadilisha mabomba ya maji machafu, mimi nawapongeza sana ikiwa *block* namba 1, 3 na 5, hata kutia rangi! Hawa wenzetu hawawezi sasa hivi, hawana fedha majumba yamekaa tangu enzi hayajatiwa rangi, jumba lilotiwa rangi ni moja namba 10 lilomaliza hivi karibuni, ndio kidogo lina rangi. Kwa hivyo, tusiwalaumu tuwape nguvu hii wenzetu watufanyie kazi tuone maendeleo kwa wananchi wetu na kwa Zanzibar yetu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nimalizie mimi, mimi naupongeza sana mswada huu ulivyokuja kwa nia njema, nia safi kwa nchi yetu hii na naamini tutaendelea katika ukurasa wa 9 (3) (i) wamesema; "Kuuza mali, nyumba au vitu chakavu". Wamesema kabisa watauza hizi mali na nyumba chakavu. Lakini mimi nawashauri kwa sababu Mhe. waziri, aangalie zile nyumba walizokuwa wanaishi wale wenzetu sasa hivi kama kuna uwezekano basi wauziwe zile nyumba kuondosha haya matatizo, kuna watu wanakaa Mji

Mkongwe, wauziwe baadhi ya nyumba, pamoja na hizi za Kikwajuni na Kilimani, baadhi tujenge majengo mapya yanayokwenda juu ghorofa 20 ili hawa wananchi wetu wajenge imani kabisa na Serikali yetu kwa ajili ya makaazi yao wasiwe na hofu kwa mswada huu kupita wao watahamishwa.

Kwa hiyo, naomba kama inawezekana hizi nyumba chakavu wauziwe ili waweze kwenda na maisha yao na hawa shirika la nyumba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu waweze kujenga nyumba mpya kabisa na naamini wameshafika katika nchi za wenzetu kama China kuona jinsi gani walivyoendelea hawa wenzetu kwa miradi yao hii ya shirika la nyumba au miradi mbali mbali kwa kujenga nyumba za makaazi ya wananchi, kwani suala hili ni muhimu na linamgusa kila mtu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakushukuru sana naunga mkono mswada huu mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Ibrahim, tumepata ombi la dakika kama tano mpaka 10 na Mhe. Nassor Jazira.

Mhe. Nassor Salum Ali: Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana na mimi kunipa nafasi chache kabisa kwa kumalizia mjadala huu.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. waziri, pamoja na katibu mkuu na naibu katibu mkuu na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kutayarisha na kuwasilisha mswada huu muhimu wa kuanzisha Shirika la Nyumba Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar inahitaji kuwa na shirika la nyumba kwa kipindi kirefu kama walivyo wenzetu katika nchi za Afrika Mashariki. Shirika la Nyumba katika siku za mbele litatusaidia sana katika juhudi za kupatikana kwa nyumba za mkopo na za bei nafuu kwa wananchi wa Zanzibar, kwani shirika litaweza kuingia katika mikataba na mabenki mbali mbali na kuweza kukopeshwa fedha za kuendeleza kujenga nyumba za makaazi kwa ajili ya wananchi. Kwa hivyo, niseme kwamba mswada huu ni mzuri na unahitajika tukiwa kama Wawakilishi wa wananchi kuupitisha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, lakini shirika pia, litaweza kusimamia vizuri nyumba za Serikali na tunajua kwamba safari hii ni ndefu na matayarisho makubwa yanahitajika, lakini tuyaangalie kwamba hata wenzetu Tanzania Bara

walianza kama hivi katika miaka ya 1960/1970 na kwa kweli wamepiga hatua kubwa katika shirika kama hili la nyumba. Kwa hivyo, nimesema kwamba nisimame hapa ili na mimi kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na niwaombe wenzangu kwamba tuupitishe mswada huu kwa faida yetu sisi, wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, nimuombe Mhe. waziri, kwamba atakapokuja basi angalau kwa sababu baadhi ya wananchi wana wasi wasi sana na mswada huu ni vyema aje atueleze ule wasi wasi ambao wananchi wanao hususan wale wananchi ambao walipewa nyumba na mzee wetu Abeid Amani Karume. Kwa hivyo, atakapokuja atueleze na kutoa wasi wasi wananchi hawa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hata kibiashara pia kwa sababu shirika litakapoanzishwa litaweza kusimamia vyema nyumba za Serikali na kuweza kujiendesha kibiashara na kupata faida kwa Serikali na kwa faida ya Wazanzibari kwa ujumla. Kwa hivyo, nilisema niseme hayo na mimi niunge mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja chini ya kifungu 64 cha Kanuni zetu za Baraza. Naomba mjadala huu uhairishwe mpaka Jumatatu ili kutoa muda kwa waziri na watendaji wake kutuletea majibu ya kina hasa ukizingatia kwamba leo ni siku ndogo na Serikali ina mambo mengi na nina imani kwamba itakapofika Jumatatu basi itakuwa mawaziri pamoja na watendaji wake watakuwa wamejitayarisha vizuri kutupa majibu ili wananchi na sisi turidhike kuweza kuupitisha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa michango yenu mizuri na ushirikiano mlionipa tangu asubuhi hadi sasa hivi. Leo kweli ni Ijumaa, lakini taarifa aliyonipa waziri keshajiandaa na michango yote anaweza kuimaliza jioni ya leo, yeye na naibu waziri wake. Kwa hivyo, kwa kuwa leo ni siku ndogo na muda uliobakia ni mdogo, naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni, waziri atakuja kufanya majumuisho na kupitisha vifungu.

(Saa 5:13 Asubuhi Kikao kiliahirishwa hadi Saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Kikao lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhana wataala* ambaye katukutanisha jioni hii tukiwa wazima wa afya, salama na amani.

Mhe. Naibu Spika, pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache katika mswada wetu huu na nitajitahidi sana nizungumze kwa ufupi au nichangie kiufupi ili nipate nimuachie Mhe. Waziri, aendelee na shughuli yake hiyo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, naomba sana niwapongeze na niwashukuru wachangiaji wote waliochangia Rasimu hii.

Kwanza nikianzia Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano inaongonzwa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, kwa jitihada zao nzuri na mashirikiano makubwa waliyotupa mpaka ikaweza kuwakilisha mswada huu kwenye Baraza lako tukufu. Kwa hiyo, tunawashukuru na tunawapongeza sana.

Vile vile, naomba niwapongeze wachangiaji wote waliochangia, imani yangu ni kwamba kufanikiwa kwa mswada huu basi ni michango yao na kufanikiwa kwa sheria hii basi ni kuipitisha. Kwa hiyo, niwaombe sana baada ya kuichangia basi kazi iliyobakia ni kutupa mashirikiano ili waweze kuipitisha sheria hii na tuanze kuifanyia kazi rasmi.

Mhe. Naibu Spika, nianze tu kwamba suala la Mhe. Ali Salim Ali, yeye anaghofu kuwa dhamira ya kuanzisha shirika inaweza kuwa nzuri, lakini utendaji ukawa sio mzuri. Naomba nikutoe ghofu kwamba Serikali iko makini katika kulisimamia suala hili naamini kwamba kukaa na kufikiria kuanzisha Shirika la Nyumba basi ni maslahi ya wananchi wa Zanzibar pamoja na Serikali yao. Kwa hiyo, Serikali itakuwa makini sana katika kulifatilia suala hili na kuhakikisha kwamba linafikia mafanikio ambayo tuliyoyakusudia.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuna Mhe. Mgeni Hassan Juma, yeye anashauri wizara ilipatie ufumbuzi suala la wananchi wanaodai kupewa nyumba na Mhe. Abeid Aman Karume na suala hili vile vile limeletwa na Mhe. Ali Salim Ali na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wao wana wasiwasi hawa watu waliopewa nyumba na Mhe. Karume je, watafikia wapi katika suala zima hili la shirika.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu naomba nimpe majibu ambayo kaanza kujibu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwamba mtu yoyote ambaye kapewa nyumba na Mzee Abeid Aman Karume basi mtu huyo katika maisha yake yote, kwanza tutafanya utafiti tuhakikishe tupate vielelezo vya kutosha kwamba kweli mtu huyo kapewa nyumba na Mhe. Abeid Aman Karume na tutakapopata uthibitisho basi mtu huyo hatonyanganywa nyumba ataishi katika maisha yake yote bila ya kutoza kodi ya aina yoyote.

Lakini baada ya kufariki yeye wale watu ambao wamo ndani ya nyumba ile wanachotakiwa kufanya ni kwamba waje kuonana na shirika letu na wafunge mkataba ili walipe kodi ya Serikali. Lakini kwa yule ambaye kapewa basi hilo halina matatizo juu yetu.

Mhe. Naibu Spika, tunaamini kwamba Wazanzibari wengi hawana makaazi ya kutosha na wanahitaji makaazi. Lakini vile vile ni kwamba kuna baadhi ya watu ambao huleta shida zao ndani ya Idara ya Nyumba kwa sababu sasa hivi bado ni idara wanakuja kwetu na wanaomba makaazi, lakini jambo la kusikitisha wanakuja na shida za kutaka makazi tunajitahidi kuwapatiwa makaazi, lakini baada ya kupewa makazi hayo wanakaa kwa muda ambao wanaokaa ndani ya nyumba hizo, lakini baada ya muda wanapopata uwezo wa kujenga nyumba zao kitendo ambacho kinachotusikitisha kwamba nyumba zile hawazirejeshi Serikalini na wanachokifanya baadhi yao basi wanatafuta watu aidha kuwakodisha au wanawatoa wengine kwa kuwapa watu kwa ajili ya kilemba.

Hili suala kwa kweli wanatusikitisha sana na sisi tunachoamini kwamba matatizo haya pindi kama mtaipitisha sheria hii na kuanza rasmi Shirika la Nyumba basi tunategemea kwamba matatizo haya yataondoka na wala hayatajitokeza tena, kwa sababu shirika hili litakuwa mamlaka ya kufatilia na itakuwa na haki ya kumjua ambaye pengine kapewa kama kilemba na kufatilia, baada ya kufatilia basi tunaamini kwamba nyumba hiyo itarejeshwa Serikalini na baada ya kurejeshwa Serikalini, mtu huyo atakachotakiwa ni kufunga mkataba na shirika na hatimae kuitumia nyumba hiyo katika misingi ya sheria.

Mhe. Naibu Spika, sina mchango mkubwa baada ya hayo niseme naunga mkono sheria hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Jaku, hongera sana kwa kuongoza *bench* la mbele.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Shukurani pekee ziwaendee

Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na makatibu wao ambao wamefanikisha mswada huu kuweza kuletwa mbele ya Baraza lako tukufu.

Vile vile, natoa shukurani kwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia na kuweza kutoa michango yao ambayo imedhihirisha kwamba mswada huu ulikuwa unasubiriwa kwa hamu na Wajumbe na wana hamu kubwa wananchi na Taifa kwa jumla.

Napenda kuwashukuru tena Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao ya kujenga na kuboresha mswada huu. Napenda kuwatambua Wajumbe waliochangia Baraza lako tukufu ambao ni kumi na nane walichangia kwa kuzungumza na mmoja alichangia kwa maandishi wa kwanza:

(1) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi
(2) Mhe. Ali Salim Haji
(3) Mhe. Mgeni Hassan Juma
(4) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
(5) Mhe. Hija Hassan Hija
(6) Mhe. Ashura Sharif Ali
(7) Mhe. Moh'd Haji Khalid
(8) Mhe. Saleh Nassor Juma
(9) Mhe. Haji Masoud Hamad
(10) Mhe. Fatma Mbarouk Said
(11) Mhe. Abdallah Juma Abdallah
(12) Mhe. Rufai Said Rufai
(13) Mhe. Panya Ali Abdalla
(14) Mhe. Hassan Hamad Omar
(15) Mhe. Marina Joel Thomas
(16) Mhe. Hussein Ibarahim Makungu
(17) Mhe. Nasor Salim Ali
(18) Mhe. Naibu Waziri wa Wizara **ya** Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Aliechangia kwa maandishi ni Mhe. Mohammed Said Dimwa, yeye alichangia michango yake kwa maandishi.

Michango yote hii naipokea na kwa kweli nashukuru sana kwamba mmeonesha matumaini ya huu mswada kuukubali na wote wameukubali kabisa mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi alieleza ushauri aliopewa na Kamati ya baadhi ya vifungu ambayo kwa kweli imefanya kazi

kubwa sana Kamati katika kurekebisha mpaka lugha katika hivi vifungu, kwa hivyo, tunawashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwenyekiti, ameomba kwamba tuzungumze habari za watu waliopewa nyumba na marehemu mzee Abeid Aman Karume, hili naliweka mwisho nitalizungumza. Mhe. Naibu ameanza kuligusa lakini lina vifungu vingi, ndio nimeeleweka mwisho wakati ukifika nitakuja kulizungumza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Salim Ali, yeye ameshaeleza ghofu ambayo Mhe. Naibu Waziri, ameshamtoa ghofu hiyo na Mhe. Ali Salim, amezungumzia suala juu ya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi kwamba lazima watumiaji kodi wawe wana ukomo kama walivyozungumza Wajumbe wengi. Kwa hivyo, katika kifungu hiki tunaongeza maneno kwa kipindi chengine kimoja akimaliza kile basi chengine kimoja tutawateuwa wafanyakazi hao, akimalizika tena ndio basi tutatoa wengine wapya.

Mhe. Naibu Spika, halafu Mheshimiwa ameulizia juu ya suala la matatizo ya akili, sisi tutakirekebisha kifungu hiki kama walivyouliza wengine kwamba atapoteza ujumbe wa Kamati ikiwa atapata maradhi ya akili tutaweka hivi. Ametaka kifungu namba 12 kifanyiwe marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kulikuwa kuna waraka hapa wa marekebisho tumeutoa ambao kifungu hiki tayari alipouliza tayari kimeshafanyiwa marekebisho katika ile hoja iliyofanywa na Kamati kuleta kile kifungu sasa kina marekebisho tayari na tumelenga pale alipokuwa anapataka yeye.

Halafu amezungumza juu ya suala la je, ikiwa Mwenyekiti anaumwa atatoa vipi hiyo *fatwa* ya kufanya kikao chengine au kumpa mtu. Kwa kweli hili litaamuliwa katika Kanuni mswada huu ukipita tutatengeneza Kanuni, Kanuni itaeleza namna gani atapatikana huyo mtu. Kwa hivyo, wao watamteuwa mtu atakuwa kama Makamu Mwenyekiti ambaye ameshateuliwa kwa mujibu wa Kanuni za Sheria hii. Lakini hatukumuweka moja kwa moja katika sheria.

Vile vile, ameomba kwamba kifungu cha 16 kirekebishwe na hichi pia nampa taarifa, akitizama waraka wa marekebisho tayari kimesharekebishwa na kifungu cha 22(1), nacho pia katika waraka wa marekebisho kimerekebishwa na kimelenga kama alivyotaka. Kifungu cha 24 (2) hiki ni kweli kifungu kilikuwa kina makosa na tumefanya marekebisho vile vile kama ilivyotaka Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na yameenda maombi aliloomba Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, ametoa pongezi kwangu pamoja na wafanyakazi wangu wote, tumepokea hizo pongezi na tutajitahidi kuwa watekelezaji zaidi baada ya kuwa hivi, amesema sifa za Mwenyekiti na Wajumbe zitenganishwe kifungu cha 9.

Ni kweli katika maneno ya pembeni sifa za Mwenyekiti na Wajumbe zimeandikwa pamoja. Lakini ndani ya kifungu sifa za Mwenyekiti zipi 9 (1) na za Wajumbe zimewekwa kwenye kifungu cha 9(2), kwa hiyo, utakuja zimejitegemea. Kifungu cha 15 kimeeleza vikao vya bodi tafsiri ya kiswahili na kiengereza ziwe sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, tunaupokea ushauri huu na kimefanyiwa marekebisho maneno ya pembeni *marginal note* na yatasomeka vikao vya bodi.

Mhe. Naibu Spika, hili suala la nyumba waliopewa na mzee Karume nimesema nitalizungumza baadae. Ametoa ushauri kwamba moja katika bodi ni kusikiliza malalamiko ya wapangaji. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa kwa vile vipo vyombo vinavyoshughulikia kisheria malalamiko na kesi za wapangaji ni vyema malalamiko na kesi za wapangaji zikashughulikiwa huko. Hata hivyo, kwa mujibu wa sheria hii bado itakuwa na nafasi ya kusikiliza malalamiko ya wapangaji.

Kuhusu *account* iangalie tafsiri ya kiswahili na kiingereza kifungu cha 40 kimefanyiwa marekebisho katika *marginal note* na kitasomeka *account* baada ya *current account* kwa mswada wa kiingereza. Mhe. Mgeni Hassan Juma, anasisitiza matumizi yote ya fedha wafate sheria za nchi na anaomba hili lijitokeze wazi katika sheria. Sheria hii tayari imezingatia mapendekezo kama yalivyotolewa na Mhe. Mgeni Hassan Juma na imeelezwa wazi katika kifungu cha 43 (2) cha sheria hii ukiisoma utaikuta.

Mhe. Makame Mshimba, yeye amepongeza juu ya mswada huu kuwasilishwa Barazani kwa wakati huu. Pongezi zimepokelewa anauliza kwamba kuna watu wamepewa nyumba na marehemu mzee Karume nasema hili nitalizungumza mwisho kwa sababu suala hili tayari limeshapatiwa ufumbuzi. Amejenga ghofu ya kutokea mgongano wa sheria katika sheria hii na Sheria za Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Namuhakikishia kwamba hakuna mgongano wowote wa kisheria katika mamlaka mbili hizi na kila taasisi itafanyakazi kwa mujibu wa sheria ya uundwaji wa taasisi husika. Anashauri kwamba sifa za Mwenyekiti ziwekwe wazi na anashauri angalau awe ametembea sana.

Mhe. Naibu Spika, hili si la Mwenyekiti, vile vile na nitaliweka mwisho na nitakuja kulizungumza kwa sababu limetolewa mapendekezo mengi kabisa juu suala hasa la kitaaluma.

Mhe. Makame Mshimba, ameshauri Waheshimiwa Wawakilishi wawe miongoni mwa Wajumbe wa Bodi. Hili sio baya, kitu muhimu ni kwamba zile sifa kwa sababu siku hizi unapounda bodi, Wajumbe wa Bodi wanatakiwa na sifa maalum. Kwa hivyo, wakitimiza hizo sifa hakuna matatizo yoyote wataingizwa katika bodi. Ameshauri kwamba shirika lifanye kazi kwa kujitegemea lisiingiliwe ingiliwe, nakubaliana na ushauri wake.

Mhe. Hija Hassan Hija, ameshauri kifungu cha 2, neno "kutwa" litoke na liwe "kuchukuwa". Ushauri wake tumeupokea na litasomeka "kuchukuwa" baada ya "kutwaa". Mheshimiwa ameuliza majengo yaliokuwa ya idara yanajulikana.

Mhe. Naibu Spika, nyumba zote ambazo ziko chini ya Idara ya Nyumba sasa hivi zinajulikana na kwa ufupi ni kwamba nyumba zote zilioko Unguja na Pemba ni nyumba elfu 2072, hizi ni mali ya idara na hizi ziko Michenzani, Kikwajuni, Kilimani, Mombasa "A" Mombasa "B" Saateni, Bet- el Ras, Gamba, Makunduchi, Mpapa Bambi, Mazizini Nyumba za viongozi, Mazizini nyumba ndogo ndogo, Mji Mkongwe, Madungu, Macho Manne, Mapinduzi, Mtemani, Micheweni, Chake Chake, Wete, Mkoani, Maziwa Ngombe, Kiuyu Mbuyuni pamoja na Kengeja.

Mheshimiwa, ameshauri kwamba utaratibu wa kumteuwa Mwenyekiti taaluma iwekwe wazi anashauri isipungue Stashahada, hili nimesema nitalijibu baadae. Halafu yaongezwe maneno mwisho yatakayosomeka kwa mujibu wa Kanuni ushauri wake tunaupokea katika kifungu cha 14(5).

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa, ameshauri kwamba kifungu cha 18 kifutwe kwa sababu kinafanana na kifungu cha 14. Tunashauri kiendelee kubaki kwa vile vifungu hivi vinazungumzia kuwaalika makundi mawili tafauti, kifungu cha 14 (4) kinazungumzia kumualika mtu mwenye taaluma kwenye kikao cha bodi wakati kifungu cha 18 kinazungumzia kuwaalika watu wa kawaida ikiwa ni pamoja na wapangaji kwenye vikao vya bodi pale panapohitajika.

Mhe. Ashura Sharif Ali, ametoa pongezi kwa Mhe. Waziri, tunazipokea hizo pongezi na pia kwa wafanyakazi kwa mswada huu. Anashauri Ardhi itengwe kwa ajili ya makaazi. Hiyo ndiyo maana tukawa tunatayarisha mpango wa matumizi ya ardhi tujue ardhi ya makaazi ni ipi, ya kilimo ipi na zile nyengine zinazotumika kwa ajili ya ufugaji na mambo mengine hiyo tayari tunaifanyia

kazi na muda si mrefu tutaileta katika Baraza hili *land use plan* ambayo imeshakubaliwa sasa hivi.

Anashauri kifungu cha 6 (2) sehemu ya mwisho kiengezwe neno ikiwa kama atapoteza sifa. Napenda kumjibu Mheshimiwa kuwa hivi vipindi vya miaka minne, minne tayari ni vipindi vya kutathmini na kuangalia utendaji wa Mkurugenzi. Bila shaka yule anayefanya kazi katika kipindi cha kwanza akionekana si barabara hatateuliwa tena mara ya pili itakuwa kishajulikana kwamba huyu hana sifa. Lakini akiendelea kuwa na sifa ndiyo atakwenda kuteuliwa tena hiyo mara ya pili.

Halafu Mheshimiwa amesema kufilisika kulikokusudiwa katika kifungu 12 (e) ni kule kufilisika ambako kumetangazwa na Mahakama kwa mhusika. Kuna utaratibu wa mtu akifilisika anatangazwa rasmi na Mahakama kwamba huyu mtu *muflis* na mtu huyu anakuwa mara nyingi hapati nafasi nyingi sana na huu uamuzi unatoka Mahakamani kabisa. Alitaka ufafanuzi wa neno amefilisika, ni hivyo nilivyokwisha kutaja. Anapongeza mikataba kupitiwa upya, tunakubali na tunapokea ushauri huo.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, yeye anaomba shirika liwe makini na kufanya kazi kwa uadilifu. Ushauri tunaupokea na tutajitahidi kuwaomba wafanyakazi wawe hivyo.

Amezungumzia kifungu cha 7(2) kuwa shirika litajenga nyumba na nyumba ni gharama. Anashauri shirika lijenge nyumba kwa viwango kuepusha maafa. Ushauri umepokelewa na shirika litakaloanzisha litazingatia hayo.

Shirika litaanza kazi katika hali ngumu na nyumba nyingi ni mbovu. Anashauri shirika liwe makini kuhakikisha kila mpangaji analipa kodi kwa wakati na anashauri pia mtaji uliopo utumiwe vizuri na pia, shirika litafute eneo kwa ajili ya kujenga nyumba za kisasa. Ushauri wake tunaupokea na tunamhakikishia kwamba shirika litakaloundwa litafanya kazi zake kwa umakini ikiwa ni pamoja na kutafuta eneo kwa ajili ya kujenga nyumba za kisasa.

Mhe. Saleh Nassor Juma, pia amempongeza waziri pamoja na watendaji tunashukuru sana tunapokea na anasema kifungu cha 9 (1) awe Mzanzibari wa kuzaliwa. Sheria hii inazungumzia Mzanzibari anayetambulika kisheria.

Vile vile, kifungu cha 6 (2) kuwa elimu ya mkurugenzi mkuu iwe *degree of master* na uzoefu wa miaka mitano. Kwa mahitaji ya shirika litakaloundwa kiwango cha elimu cha Shahada ya Kwanza na hiki ni cha kuanzia, kama yupo wa Shahada ya Pili, wa Shahada ya Tatu na Shahada ya Kwanza na

elimu zao na uzoefu wao upo tofauti, basi bila shaka yule wa Shahada ya Tatu ndiye atakayechukuliwa kuliko yule wa Shahada ya Kwanza. Hapa ni kama mahali ambapo tunaanzia tu. Shirika litatoa nafasi kwa watendaji wake kujiendeleza kielimu akiwemo mkurugenzi mkuu, ikiwemo kuwapeleka ziara ya kimasomo nchini China kama alivyopendekeza Mheshimiwa.

Mhe. Hamad Masoud Hamad, anauliza katika kutengenezwa mswada huu, idara imeangalia wapi mashirika yenye mafanikio. Idara imejifunza kutoka kwa wenzetu wa Shirika la Nyumba la Taifa la Tanzania *(NHC)* na lilipeleka watendaji wa fani mbali mbali kujifunza kupata mafunzo ya muda mfupi. Pia, wizara ilifanya jitihada ya kuipeleka Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi iliyopita na ya sasa kwenda Shirika la Bima la Taifa kujionea wenyewe mafanikio waliyopata wenzetu.

Pia, idara ilipata nafasi ya kujifunza masuala ya Shirika la Nyumba kwa kufanya ziara za kimafunzo nchini Seychelles.Unajua Seychelles katika suala hili wameendelea sana wale, wamejenga nyumba nyingi sana kule na wananchi wanafaidika na ujenzi ule. Kwa hivyo, idara ilikwenda huko na kujifunza namna walivyofanya kazi na kujifunza mafanikio yao pamoja na changamoto zao.

Ameuliza je, idara wana *assets* za kutosha au Serikali italipa shirika mtaji wa kutosha. Idara inazo *assets* za kutosha kama zilivyoainishwa hapo juu. Idara inao wafanyakazi wazuri na wenye taaluma katika fani mbali mbali na shirika litakapoanzishwa litaajiri wataalamu kwa mujibu wa mahitaji ya shirika.

Mhe. Hamad Masoud Hamad, alisema kwamba pana wataalamu wengi sasa hivi wa masuala ya ujenzi hapa Zanzibar ambao hao ndiyo tunaokusudia tuwatumie katika kuanzisha shirika hili la nyumba ambalo tunalo.

Ameuliza miongoni mwa kazi za shirika ni usimamizi, ujenzi na ushauri elekezi, ana wasi wasi kuwa hili litaleta matatizo. Shirika litakuwa na uwezo kuwa mjenzi au mshauri elekezi au msimamizi wa ujenzi. Hapo tunaomba ieleweke kuwa katika mradi mmoja shirika linaweza likafanya kazi moja tu kati ya hizo, haliwezi kufanya kazi zote hizi katika mradi mmoja.

Shirika lilisajiliwa katika bodi ya mkandarasi kwa mujibu wa sheria husika na ikitokezea kazi za nje binafsi shirika litashindania tenda, hii ni kwa lengo la kuongeza mapato ya shirika.

Anashauri baada ya neno "*building construction"* iwekwe neno "*civil engineering"*. Katika kifungu cha 6 (1) ya kiingereza kuna maneno *"In the field of building construction"*. Kimsingi sentensi hii inajumuisha eneo pana

katika taaluma ya ujenzi. Kwa maana hiyo, *civil engineering* anaingia moja kwa moja, *architect in building* anaingia, pia *QS* anaingia, kwa mantiki hiyo hatuoni haja ya kifungu hiki kukifanyia marekebisho.

Anashauri bodi isipewe kazi ya kukopa tu, pia ipewe kazi ya kuuza. Masuala ya kukopa na kuuza yameainishwa katika sheria hii kifungu cha 3 (2)(d) na pia, kifungu cha 7 (3)(i), kuhusu Sifa za Mkurugenzi Mkuu na Mwenyekiti wa Bodi ziainishwe atafutwe Mwenyekiti mwenye *knowledge* ya kutosha. Sheria imezingatia hayo katika kifungu cha 6 (1) na 9 (1) vile vile.

Mhe. Fatma Mbarouk Said, amempongeza waziri nashukuru sana kwa pongezi zako Mheshimiwa pamoja na wafanyakazi wangu ambao wamepokea pongezi hizo na wamefurahi kusema kweli.

Anashauri mikutano ya bodi iwe minne. Sheria hii imeeleza vikao vya bodi vinne kwa mwaka angalia kifungu cha 15 (1).

Kifungu cha 38 (a) Mheshimiwa, anataka maelezo juu ya fedha zilizotajwa katika kifungu hiki. Kifungu hiki kimekusudia fedha zitakazopatikana katika utekelezaji wa majukumu ambazo ni makusanyo ya kodi ya nyumba za shirika, mauzo ya nyumba za shirika na kazi za ujenzi shirika itakazochukua.

Mheshimiwa, anashauri shirika liwe na akaunti zake na sio yake. Katika akaunti hizo iwe *capital account* na *deposit account.* Ushauri wake tumeupokea na katika *marginal note* kifungu cha 40 (1) neno "yake" baina ya "akaunti na ambayo" sasa itasomeka "akaunti zake". Na katika mswada wa kiingereza *marginal note* ya kifungu cha 40 neno *"current"* litaondoka na kusomeka *"account"* moja kwa moja.

Anashauri kuwepo kifungu cha ufungaji wa hesabu ya mwaka na pia, anashauri zikitungwa sheria kuwepo na Kanuni kwa maana hiyo tufanye haraka kutunga Kanuni. Mheshimiwa, sheria tayari inaelekeza masuala ya ufungaji hesabu angalia kifungu cha 43 (1) na 43 (2). Pia, kifungu 52 kinazungumzia kutunga Kanuni.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla, kwa mara mbili, tatu pamejengwa nyumba, lakini nyumba hizo zimegaiwa kwa wananchi wenye uwezo badala ya watu wa kipato cha chini. Shirika litakaloanzishwa linakusudia kujenga nyumba kwa ajili ya wananchi wa vipato vyote. Lengo la shirika ni kujenga nyumba za kutosha na kufanya nyumba zitafute watu badala ya watu kutafuta nyumba. Hiyo ndiyo jitihada tunataka tuifanye.

Anashauri kifungu cha 7 (3) kifutwe. Ni vyema kifungu hiki kikabakia kwa vile kimekusudiwa kurahisisha shirika kupata vifaa vya ujenzi kwa ajili ya miradi yake, sio kwa ajili ya kuwauzia watu zaidi. Inataka kufanya kazi ya ujenzi kwa miradi yake.

@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@@

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

(Hapa Katibu Mezani hakutumia kipaza sauti)

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumikia
Kifungu 2	Ufafanuzi
Kifungu 3	Kuanzishwa kwa shirika
Kifungu 4	Muundo wa Shirika
Kifungu 5	Mkurugenzi Mkuu
Kifungu 6	Sifa za Mkurugenzi Mkuu
Kifungu 7	Kazi za Shirika
Kifungu 8	Muundo wa Bodi
Kifungu 9	Sifa za Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi
Kifungu 10	Katibu wa Bodi
Kifungu 11	Muda wa Bodi
Kifungu 12	Kukosa Sifa
Kifungu 13	Kazi za Bodi
Kifungu 14	Kamati za Bodi
Kifungu 15	Mikutano ya Bodi
Kifungu 16	Vikao vya Dharura
Kifungu 17	Maamuzi ya Bodi
Kifungu 18	Kualika
Kifungu 19	Kujaza nafasi
Kifungu 20	Kumbukumbu za Bodi
Kifungu 21	Akidi
Kifungu 22	Maagizo na maelekezo ya Bodi
Kifungu 23	Maslahi ya Wajumbe wa Bodi
Kifungu 24	Uwezo wa kukasimu
Kifungu 25	Mahitaji yanayohitajika na Waziri
Kifungu 26	Uwezo wa kuingia mikataba
Kifungu 27	Upangaji wa kodi

Kifungu 28	Mikataba ya upangishaji iliopo
Kifungu 29	Malipo ya kodi
Kifungu 30	Adhabu ya kuchelewa kulipa kodi
Kifungu 31	Kodi na adhabu iliyotolewa itakuwa ni deni
Kifungu 32	Mpangaji kumpangisha mtu mwengine, kumpisha na mabadiliko
Kifungu 33	Kuvunja Mkataba wa upangaji
Kifungu 34	Taratibu za kuvunja Mkataba
Kifungu 35	Siri
Kifungu 36	Taarifa za udanganyifu
Kifungu 37	Uwezo wa kuingia na kufanya ukaguzi
Kifungu 38	Fedha na rasilimali za Shirika
Kifungu 39	Uwezo wa kukopa na kudhamini mikopo
Kifungu 40	Akaunti
Kifungu 41	Fedha kwaajili ya Uwekezaji
Kifungu 42	Bajeti
Kifungu 43	Hesabu na Ukaguzi
Kifungu 44	Ripoti ya mwaka
Kifungu 45	Kinga ya Wajumbe
Kifungu 46	Makosa
Kifungu 47	Makosa yanayofanywa na kampuni
Kifungu 48	Kosa la Muajiri au Mkuu
Kifungu 49	Taarifa ya Amri na Muongozo
Kifungu 50	Wajibu wa kuthibitisha
Kifungu 51	Msamaha
Kifungu 52	Waziri kutunga Kanuni
Kifungu 53	Kubakisha

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeipitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar, 2014

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwashukuru kwa kazi nzuri tuliyofanya na kuweza kupitisha mswada wetu huu ambao ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Kabla sijaahirisha kikao chetu nina matangazo matatu.

Tangazo la kwanza, nimeletewa taarifa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwamba kesho kutakuwa na mahafali katika Chuo chao cha Afya Mbweni, saa 3:00 asubuhi. Kwa hivyo, tunaalikwa wote tushiriki katika sherehe hizo.

Tangazo la pili, wale wote Wajumbe wanaokwenda shamba Chambani wanaambiwa gari itakuwepo nje, tukimaliza kikao ipo tayari kwa kuwapeleka. Wale wanaojitegemea wameshajieleza wenyewe.

Tangazo la tatu, nimeletewa taarifa na Msaidizi Meneja wa timu yetu ya Baraza la Wawakilishi kwamba mazoezi rasmi yanaanza kwa Waheshimiwa wote pamoja na vijana wetu kesho uwanja wa Mao-Tse-Tung saa 12:00 asubuhi ili tarehe 8/11/2014 tunacheza mechi ya marudiano na wale rafiki zetu wa Dar es Salaam. Kwa hivyo, kwa kule tuliwafunga, kuja kutufunga hapa itakuwa aibu, zoezi tufanye kwa pamoja ili ushindi wetu tuweze kuutetea. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, naahirisha kikao chetu hichi hadi siku ya Jumatatu ya tarehe 27/10/2014 saa tatu za asubuhi.

(Saa 11.53 jioni Kikao kiliahirishwa hadi tarehe 27/10/2014 saa 3.00 asubuhi)